# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Februari 2, 2025 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581940

www.ippmedia.com

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com




UKURASA WA 21

**MBWEMBWE ZATAWALA NEYMAR AKITUA SANTOS**

UKURASA WA 3

**Mkuu** wa shule adaiwa kujiua kwa sumu

MKUU wa Shule ya Sekondari ya Chambo katika Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, Zaharani Patrombeyi...

UKURASA WA 5


**Wafungwa**, mahabusu kuwekewa vituo vya uboreshaji daftari wapigakura

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kwa mara ya kwanza inaanza uandikishaji wapigakura kwa wafungwa, wanafunzi...

UKURASA WA 7

KONA YA AFYA:

**Sahani** ya lishe bora wagonjwa maradhi ya figo



KUTHIBITI ugonjwa sugu wa figo ni changamoto kubwa inayohusu wagonjwa na watoa huduma...

**W'biashara 1,520 warejeshwa Soko Kuu Kariakoo**

UKURASA 2

# Neema yaja kwa walimu

• **Serikali** yaahidi kupitia maslahi, kuongezewa ujuzi...

*Endelea ukurasa 2*




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Matiku, mfano wa ufunguo wa gari kwa ajili ya huduma ya afya inayotembea (Mobile Clinic) kwa wilaya za Sikonge na Uyui, yaliyotolewa na Jakaya Kikwete Foundation, chini ya ufadhili wa Kampuni ya SC Johnson Family, ya nchini Marekani, hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma. **PICHA: IKULU**



RIPOTI YA UCHUNGUZI- 2

## Mifumo, usimamizi mbovu wa sheria ulivyo chanzo cha rushwa barabarani

UK. 4

**MICHEZO** SIMBA, TABORA UTD MWISHO WA TAMBO UK.24 **KATUNI** UK.6

# Wafanyabiashara 1,520 warejeshwa Kariakoo

**Na Restuta James**

MAJINA ya wafanyabiashara 1,520 watakaorejea katika Soko Kuu la Kariakoo, jijini Dar es Salaam yametajwa na kutakiwa kwenda kujisajili kuanzia kesho hadi Ijumaa Februari 7, mwaka huu.

Kaimu Meneja Mkuu wa Shirika la Masoko ya Kariakoo, Mwinga Luhoyo, katika taarifa yake kwa umma juzi, alimtaka kila atakayeona jina lake, kufika katika ukumbi wa Arnatoglu kwa ajili ya kujisajili kwa kujaza fomu na kufuata taratibu zinginezo za kiupangaji.

Alisema soko hilo lipo katika hatua za mwisho za kurejea kwenye biashara baada ya kukamilika kwa ujenzi na ukarabati.

"Ili shughuli hizo zirejee, shirika linatangaza kwa umma orodha ya wafanyabiashara 1,520 ambao wamehakikiwa na kamati iliyoundwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mfanyabiashara anakumbushwa kufika akiwa na kitambulisho cha Taifa na namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN)," alisema.

Katika orodha ya awali, wafanyabiashara 1,170 walirejeshwa na orodha ya pili waliorejeshwa ni 350.

Maeneo ambayo wafanyabiashara hao wamerejeshwa na idadi yao kwenye mabano ni wasaidizi soko dogo (29), wasaidizi soko dogo mzunguko (49), walionunua maeneo kutoka kwa waliokuwa wapangaji (33), waliokuwa eneo la promosheni (45), wafanyabiashara waliofariki dunia na maeneo yao kurithiwa (36) na majina ya wasaidizi (45).

Wengine ni wenye mitaji yao soko dogo ndani (45), majina ya wafanyabiashara waliopangishwa maeneo ya biashara (70), wauza mbogamboga shimoni (38) na wauza ndizi jumla soko la shimoni (15).

Pia wamo waliokuwa kwenye vigoli sokoni Kariakoo (98), soko la wazi (194), soko dogo mzunguko (242), shimoni (322), soko la ndani (152) na soko kuu (163).

Juzi, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Masoko ya Kariakoo, Hawa Ghasia, alisema wafanyabiashara 366 wanadaiwa zaidi ya Sh. milioni 358 na kwamba, hawatarejeshwa hadi watakapolipa madeni yao.

Soko la Kariakoo limekarabatiwa na kuongezwa maeneo mapya baada ya kuungua Julai 10, 2021 na kuteketeza mali za wafanyabiashara. Aidha, serikali imelikarabati kwa Sh. bilioni 28.03.

Katikati ya wiki, Rais Samia Suluhu Hassan, alipokutana na kula chakula cha mchana na watu walioshiriki uokoaji kwenye jengo la ghorofa lililoporomoka Kariakoo, Novemba 16, 2024, alisema chanzo cha kuungua kwa soko hilo ni ili kupoteza ushahidi wa kilichokuwa kinaendelea sokoni hapo.

"Nilikuja Kariakoo na baaada tu ya kuondoka, kesho yake mkalitia moto. Baada ya kuzisema changamoto za uongozi uliokuwapo na mambo yaliyokuwa yakifanyika katika soko na kuvitaka vyombo vinavyohusika kufanya uchunguzi ndani ya soko, ili kupoteza ushahidi mkalichoma moto, lakini kwa ujasiri nikaamua kulijenga tena," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema juzi kwamba soko hilo litaanza kufanyakazi kwa saa 24 kuanzia Februari 22, mwaka huu.




Basi la Kampuni ya Esther Coach likiwa limeligonga gari dogo aina ya Rv4 Moshi mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia atangaza neema kwa walimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amezindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 na kuahidi kuwa serikali itapitia upya maslahi ya kada ya walimu ili kuipa hadhi inayostahili.

Pia amesema serikali itaendelea kuajiri walimu wenye sifa na kuwapa mafunzo stahiki ili waendane na mwelekeo wa sera hiyo.

Akizungumza jana jijini hapa, Rais Samia alisema pamoja na uhitaji wa rasilimali na miundombinu ya elimu, kiungo kikubwa katika utekelezaji huo ni mwalimu.

"Kwa maoni yangu (mwalimu) ndiye kiongozi wa elimu, hivyo katika maboresho haya, lazima mwalimu awe katikati ya mduara wa maboresho yetu. Tutapitia upya maslahi ya kada ya walimu nchini ili kuipa hadhi inayostahili kama mama wa taaluma zote duniani.

"Niitake TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) kuandaa mkakati wa kutekeleza sera hii kwa upande wa miundombinu," alisema.

Rais Samia aliziagiza Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuwezesha na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa sera na mitaala mipya ili kuleta matokeo yaliyokusudiwa.

Kuhusu sera hiyo, alisema elimu itakuwa ya lazima kutoka miaka saba na kuwa 10 na kwamba hiyo ilitokana na wanafunzi kumaliza elimu ya msingi wakiwa na umri wa miaka 13, hivyo kukosa sifa ya kuajiriwa na kujiajiri.

Pia alisema wanakuwa hawana elimu ya ufundi hivyo kwa sasa kupitia sera hiyo, itamwezesha kijana kuingia kwenye uzalishaji.

Alisema sera hiyo inajibu hoja ya muda mrefu ya kuweka mfumo wa kutoa na kurasimisha ujuzi unaopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo ulioko.

Aidha, alisema somo la ujasiriamali litakuwa la lazima kwa kila mwanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne, ili kumpa misingi ya biashara na kujifunza Lugha za Kiingereza, Kichina, Kifaransa na Kiarabu, kwa kuwa ndizo zinazoendesha uchumi duniani.

Awali, Rais Samia alitaja mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kuanzia mwaka 2021 hadi 2024 yakiwamo serikali imejenga shule za msingi 1,649 na shule mpya za sekondari 1,042 na zimeongeza fursa za elimu kwa watoto, huku vyuo vya ufundi stadi (VETA) vikijengwa kwenye mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe na Rukwa.

Ujenzi wa vyuo vya VETA, alisema unaendelea kwenye mkoa wa Songwe na wilaya 64 na kwamba uwekezaji huo unawapunguzia mzigo wananchi waliokuwa wanalazimika kusafiri kwenda wilaya zingine kutafuta ujuzi.

Alisema bajeti ya mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka Sh bilioni 467 hadi 787 na wanufaika wameongezeka kutoka 149,508 hadi 220,376 mwaka 2023/24.

Hata hivyo, Rais Samia alisema idadi ya wasiojua kusoma na kuandika imepungua kutoka asilimia 70 mwaka 1960, hadi sasa wanaojua kusoma na kuandika ni asilimia 83.

Kuhusu teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), alisema ni lazima kuendana na mabadiliko ya teknolojia kwa kuwaandaa vijana kuwa na ujuzi wa masuala hayo na kuangalia matumizi hayo yasiwapeperushe na utovu wa maadili.

"Mbele yetu ninaona mahitaji makubwa ya ajira kwa vijana yataendelea kuongezeka mbele ya safari kwa sababu kubwa tatu, ambazo ni kasi ya mabadiliko ya teknolojia itakayosababisha baadhi ya kada kukua na zingine kutoweka na zile zitakazosalia hazitahitaji watu wengi," alisema.

Alitaja sababu nyingine ni utandawazi na ongezeko la idadi ya watu isiyoendana na kasi ya ukuaji wa uchumi kwa ukuaji wa asilimia 3.2 kwa mwaka ifikapo 2044, idadi ya watu nchini itakuwa milioni 123.

"Ninachokiona mbele kinahitaji tuwe na maandalizi ya kutosha kwa kuzingatia ubora wa elimu yetu kwa kutoa elimu bora zaidi na kuandaa vizuri zaidi vijana wetu kumudu stadi muhimu zitakazowawezesha kuajiriwa au kujiajiri," alisema.Rais Samia alisema utekelezaji wa sera umeanza kuonesha mwelekeo mzuri kwa kuwajengea umahiri na ujuzi vijana kwenye ufundi.

"Wataalamu wetu wamechambua vizuri mwenendo wa uchumi wetu, mwelekeo wa dunia, kasi ya maendeleo ya dunia na kujifunza kutoka kwa wenzetu. Dhamira yetu ni kumwandaa kijana anayejiamini na mwenye nyenzo stahiki kukabiliana na ushindani na anufaike kiuchumi," alisema.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema sera hiyo itawezesha kubadilisha mfumo wa elimu ili kuzalisha nguvu kazi yenye ujuzi wa teknolojia.

Alisema utafiti unaonesha sera ya elimu haiakisi mabadiliko ya teknolojia, kunakuwa na ukosefu mkubwa wa ajira kwa sababu nguvu kazi isiyokuwa na ujuzi inazalishwa kwa wingi kuzidi mahitaji.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema asilimia kubwa ya mambo yaliyokuwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ambayo ilizinduliwa mwaka 2015, hayakutekelezwa na kumpongeza Rais Samia kwa kufanikisha uboreshaji wa sera na mitaala mipya.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Ushirikiano wa Elimu Duniani (GPE), Rais Mstaafu Jakaya Kikwete, alisema bodi ya shirika hilo kuanzia mwaka 2013 hadi sasa, imechangia miradi ya maendeleo ya elimu yenye thamani ya Sh. bilioni 518.

Alisema ukaguzi uliofanyika na shirika hilo kwenye miradi hiyo nchini, umeridhika kuwa fedha hizo zinatumika vizuri na ndio maana wameahidi kuendelea kushirikiana na Serikali katika awamu nyingine ya tatu.

Kikwete alisema tayari mazungumzo ya awali katika awamu ya tatu yameanza kati ya serikali na GPE ambapo Dola milioni 88.56 zimeshatengwa na nyingine Dola milioni 50 ziko tayari kujumuishwa kwenye mpango huo.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema katika kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani na kuwapo na ubora wa elimu inayotolewa Bunge lipo tayari kufanya marekebisho ya sheria zitakazoonekana haziendani na sera hiyo mpya.

Alishauri baada ya kuzinduliwa kwa sera ni muhimu kuangalia masomo ambayo hayahitajiki tena kwa kuwa watoto wanauwezo wa kufahamu bila kufundishwa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Leila Mohamed Musa, alisema kwa upande wa Zanzibar, mapitio ya mtaala wa mafunzo ya amali yameanza ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sera na kwamba, matayarisho ya mafunzo kwa ajili ya walimu yamekamilika na kuanza kutolewa.

# Ajali basi na gari ndogo yaua watatu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WATU watatu wamepoteza maisha papo hapo, baada ya gari ndogo kugongana na basi katika ajali iliyotokea eneo la Kanani, Kiborlon, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Simon Maigwa, alisema ajali hiyo imetokea jana saa 12:45 asubuhi na kuhusisha gari lenye namba T 592 EKU Toyota RAV 4 lililogongana na basi aina ya Yutong lenye namba za usajili T 612 EGV, mali ya Kampuni ya Esther Luxury Coach, ambalo wakati huo lilikuwa likitokea Arusha kwenda Dar es Salaam.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa Toyota RAV4, Paul Sita (25), mkazi wa Dar es Salaam, kujaribu kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari.

“Sita alikuwa amepakia abiria wawili, Exaud Elipokea Mbise (65), mkazi wa Arusha na Apaikunda Ayo (61), mkazi wa Arusha waliokuwa wakitokea Dar es Salaam,” alisema.

Kamanda Maigwa alisema miili imehifadhiwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, huku akiwataka madereva kutii sheria za usalama barabarani, kwani ajali zinaepukika.

# Chuki hasi yabainika kuua kwa kasi

**Na Pilly Kigome**

WATAALAM wa afya wamebainisha kwamba ugonjwa wa chuki hasi ni moja ya ugonjwa hatari wa kuambukiza na unaoleta madhara na kuuwa kwa kasi katika jamii.

Mtaalamu wa Maendeleo ya Binadamu na Mbobevu wa Afya Bora ya Akili, Dk. Mayrose Majinge, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea Siku ya Tuzo za Kizalendo.

Dk. Majinge alisema ugonjwa huo unamaliza na kuua kwa kasi ya juu bila kujua na wengi wao hawatambui kama wanasumbuliwa nao, hali inayofanya kushindwa kujitibia na kupata suluhu ya matibabu na kupona. Alisema ugonjwa huo unaua kwa kasi kubwa kuliko magonjwa hatari duniani na kupunguza kinga ya mwanadamu kwa haraka.

Mtaalamu huyo alifafanua chuki yaweza kuwa hasi au chanya kulingana na namna inavyotumika na kuchukuliwa, huku akitolea mfano wa mtu anapata maambukizi kupitia rushwa, vurugu, ubaguzi wa rangi, kutovumilia mambo au matukio ya unyanyasaji wa kijinsia.

Alisema jopo la wataalamu waliofanya utafiti walibaini wengi wanakumbwa na ugonjwa huo kutokana na ukosefu wa upendo miongoni mwa mtu na mtu katika jamii iliyowazunguka ikiwamo kuchukiana au kutokupendana.

Alisema kutokana na hali hiyo huku Watanzania wengi wakionekana kuwa ni waathirika wameamua kuja na tuzo uzalendo zitakazoweza kusaidia watu kupendana ili kuondoa chuki baina ya mtu na mtu pasipo sababu.

“Unakuta mtu anamchukia mwenzie bila sababu za msingi, mwingine anajikuta anatamka kabisa fulani simpendi. Huyu ana viashiria vyote kuwa ni mgonjwa wa chuki, asipojitibia kwa wakati anajikuta ugonjwa huo unammaliza pasipo kujua,” alisema.

“Februari 13, mwaka huu, viongozi mbalimbali wa kitaifa, watu mashuhuri watakutana ili kutoa elimu ya kujitibia na kukabiliana na mmomonyoko wa maadili na kuepukana na chuki hasi.

Baada ya taarifa hiyo, Nipashe ilipozungumza na baadhi ya wananchi mtaani wakiwamo Joyce Peter na Peter Mathias, wote wakazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, walisema hawatambui kama kuna ugonjwa wa namna hiyo.




Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega (kulia), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa Uzinduzi wa Tuzo ya Kimataifa ya Quran Tukufu, itakayofanyika Mwezi huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam (kushoto) ni Mwenyekiti wa Tuzo hizo, Shekhe Othman Kapolo, na (katikati) ni Balozi wa Saudi Arabia, Yahya Mohamed Ukeshi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mkuu wa shule adaiwa kujiua kwa kunywa sumu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Shule ya Sekondari ya Chambo katika Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, Zaharani Patrombeyi (44), anadaiwa kujiua kwa kunywa kitu kinachosadikiwa kuwa ni sumu, huku chanzo cha uamuzi huo kikichunguzwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Janeth Magomi, alisema mwalimu huyo alikunywa sumu Januari 29, mwaka huu, saa 5:00 asubuhi.

Magomi alisema Patrombeyi hakuacha ujumbe wowote na kuwa imethibitika alikunywa kitu kinachosadikiwa ni sumu akiwa nyumbani kwake.

Alisema majirani baada ya kubaini hali hiyo, walimpeleka katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama kwa ajili ya matibabu, lakini siku mbili baadaye alipoteza maisha wakati akiendelea na matibabu.

Magomi alisema wanaendelea na upelelezi kwa kina ili kujua chanzo chake.

Kamanda Magomi aliwataka wananchi wanapokuwa na mambo mengi vichwani mwao wahakikishe wanaomba msaada wa mawazo kwa kuwafikia watalaamu wa afya ya akili waliopo na kupata msaada zaidi na kuwaomba viongozi wa dini wawafundishe watoto maadili mema na kuwakanya kutojichukulia sheria mkononi.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, walisema mwalimu huyo hakuwa na ugomvi na mtu yeyote kijijini kwao na alikuwa na ushirikiano mzuri na jamii iliyomzunguka.

RIPOTI YA UCHUNGUZI- 2

# Mifumo, usimamizi mbovu sheria ulivyo chanzo rushwa barabarani

## -Polisi yawashikilia waliofumwa katika picha mnato, jongefu

Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa KIGOMA

BAADA ya Nipashe kutoa ripoti ya uchunguzi iliyoonesha ni kwa namna gani hali ya rushwa kwa askari wa usalama barabarani ilivyokithiri mkoani Kigoma. Jeshi la polisi mkoani humo limewashikilia askari wawili wa kikosi cha usalama barabarani walioonekana katika picha mnato na jongefu wakipokea rushwa katika kituo cha ukaguzi wa magari Kazegunga.

Katika sehemu hii, ripoti inaweka wazi kilichonyuma kukithiri kwa vitendo vya rushwa kwa askari wa usalama barabarari na si tu mkoani Kigoma bali maeneo yote nchini.



Askari wa usalama barabarani katika harakati zao. **PICHA: MTANDAO**

**ASKARI WALIVYONASWA**

Taarifa iliyotolewa Januari 27, mwaka huu, na msemaji wa Jeshi la Polisi mkoani Kigoma, Philemon Makungu, ilieleza kuwashikilia askari wawili wa kikosi cha usalama barabarani walioonekana kushiriki vitendo visivyo na maadili, kinyume cha Sheria ya Usalama Barabarani kupitia video iliyorushwa katika mtandao wa kijamii wa gazeti hili.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa watuhumiwa waliokamatwa wako mahabusu na hatua za kinidhamu zinaendelea dhidi yao kabla ya hatua zingine za kisheria kuchukuliwa.

Vilevile, taarifa hiyo inaeleza namna ambavyo askari hao wamechafua taswira ya Jeshi la Polisi na kwamba jeshi hilo halitavumilia ukiukwaji wa maadili na sheria, hivyo litaendelea kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya askari wanaokiuka maadili ya utendaji kazi.

**MAONI YA WADAU**

Wadau wa masuala ya usalama barabarani wanasema Jeshi la Polisi halichafuliwi taswira na askari hao bali ni mfumo uliouokuta na kuuendeleza kutokana na mifumo mibovu ya sheria pamoja na usimamizi mbovu wa sheria zilizopo.

Aidha wanasema mifumo mibovu ya sheria ndicho chanzo cha kutozingatia sheria na kanuni za usalama barabarani, hivyo kusababisha kukithiri kwa rushwa kati ya matrafiki na madereva wa mabasi, yakiwamo ya daladala wanaotoa huduma za usafiri mkoani Kigoma na maeneo mengine nchini.

Wanasema sheria zimenyimwa meno na mamlaka zinazoshughulikia masuala ya rushwa barabarani zimeshindwa kuwashughulikia watuhumiwa kama wanavyoshughulikia makosa mengine ya jinai.

Ibrahim Sadick, Mkuu wa Kitengo cha Elimu kwa Umma kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kigoma, anasema taasisi hiyo haina mamlaka kamili ya kukamata kwa mujibu wa sheria.

Anasema hawana mamlaka ya kutuhumu, kukamata, kuchunguza na kupeleka watu mahakamani, kwa kuwa utaratibu huo unakiuka mnyororo wa haki jinai na kwamba ili kufanikisha hilo lazima awapo mtu anayeshtaki ili kuepuka uonevu.

Pia anasema hakuna mtu aliyewahi kushtakiwa kwa kosa la kutoa au kupokea rushwa barabarani kwa madai kuwa chanzo ni kukosekana kwa ushahidi.

"Hatujapokea kesi ya mtu aliyefungua madai juu ya rushwa barabarani. Malalamiko yanakuja lakini hayafunguliwi kama kesi rasmi. Tunahitaji ushirikiano wa wananchi kwa kufungua madai. Hatuwezi kuchukua hatua bila ushahidi," anasema Sadick.

Wakili Thomas Masasa kutoka Msasa Law Chamber anaangalia tatizo la mfumo kwa namna ambavyo TAKUKURU na Jeshi la Polisi wanavyopaswa kushirikiana ili kuondoa tatizo hilo.

Anasema marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Oktoba 2024, yanawapa mamlaka ya kushtaki baadhi ya makosa yanayohusiana na rushwa bila kupata kibali kutoka kwa Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali.

Anasema kuna changamoto ya vitendea kazi na idadi ya maofisa uchunguzi wa TAKUKURU kulinganisha na ile ya askari wa usalama barabarani, hivyo inakuwa ngumu kwa maofisa hao kupambana na vitendo vya rushwa barabarani.

"Ofisi nyingi za TAKUKURU zina wafanyakazi wachache. Unaweza kukuta maofisa watatu katika wilaya nzima wakati polisi wapo mara tatu yao. Watawezaje kuwakabili?" anahoji.

Anasema maofisa haohao ndio wanatakiwa wapambane na rushwa za halmashauri na taasisi zingine, hivyo inawawia vigumu kuwapo kila eneo kuzuia rushwa. Kwa mantiki hiyo, anasema wanahitaji wananchi kutoa ushirikiano dhidi ya vitendo vya rushwa barabarani.

Ripoti ya Uchambuzi wa Mfumo wa Utendaji Kazi wa Askari wa Usalama Barabarani ya Machi 2023 iliyofanywa na TAKUKURU mkoani Kigoma inabainisha kuwa baadhi ya madereva wa viongozi hukwepa sheria kwa kisingizio cha "simu moja tu."

Katika uchambuzi huo, ilionekana kuwa wanaoonewa na kuguswa na fedha ya rushwa ni wale wasioendesha magari ya wanaodaiwa kuwa viongozi wenye nyadhifa serikalini. Endapo dereva wa aina hiyo atakamatwa na kosa la usalama barabarani, akipiga simu kwa mwajiri wake mara nyingi askari aliyemkamata hupewa maelekezo ya kumwachia dereva.

Vilevile, ripoti hiyo inaonesha kuwa madereva wanaofanya kazi kwa mazoea, huamini kuwa 'pesa ya ushirikiano' inaweza kumaliza kila tatizo, hali ambayo inawakatisha tamaa askari waadilifu.

Wakili Msasa anasema madereva wamekuwa wakiwashawishi matrafiki kupokea 'pesa ya ushirikiano' kwa kuwa wengi magari yao hayajakamilika, hivyo kuliko kutoa faini ya Sh. 30,000 wanaona ni bora kutoa Sh. 2,000 kinyume cha sheria.

**SABABU KUKITHIRI**

Ripoti ya Utafiti wa Rushwa (2020) inaonesha kuwa madereva wa daladala mara nyingi hutumia rushwa kuepuka adhabu.

Dereva wa daladala za Simbo ambaye hakutaka jina lake kutajwa anasema madereva wengi hawana uelewa wa kanuni za usalama barabarani, huku wakitegemea mfumo uliopo ambao huruhusu 'ushirikiano' ili waendelee kufanya biashara.

"Tunaumizwa kwa kuwa hatujui sheria za usalama barabarani kwa hiyo mkoa umeamua kutumia huo udhaifu ili kupata pesa za ziada wakijua hakuna wa kuwashtaki," anasema dereva huyo.

Dereva Juma Juma anasema shida ya kuendelea kwa rushwa kati ya madereva wa daladala na askari wa usalama barabarani ni woga wa madereva kwa kuwa kuna kipindi wanakuwa na magari mabovu, hivyo kuwapasa kutoa 'ushirikiano' ili wasikamatwe na waendelee kufanya kazi.

"Wakati mwingine tunaogopa kwa sababu hii pesa inayotolewa haitolewi kwa siri tena na mnaweza kugombana na askari mbele ya abiria ikiwa dereva atagoma kutoa hiyo pesa, unafikiri wanajiamini na nini? Maana ndani ya gari kuna watu wengi na wao hawajali hii hali ina kitu kinachowafanya kuwa majeuri na kuhisi pesa hiyo ni haki yao" anasema Juma.

Dereva mwingine, Liberatus Dotto, anasema wanatoa rushwa kwa sababu vizuizi vimewekwa kimkakati na kufanya hivyo ni nafuu zaidi kuliko kulipa faini ya Sh. 30,000 kwa kila kosa.

Katibu wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa, Shukuru Kondo, anasema madereva mara nyingi hukwepa uwajibikaji kwa kujaza abiria kupita kiasi au kutumia magari mabovu, hali inayowafanya kutoa rushwa.

Anasema aliwahi kuwahoji madereva kwa nini wanatoa rushwa na kusababisha makosa ya usalama barabarani kwa makusudi na walimjibu kuwa rushwa haiepukiki kwa kuwa wanatafutiwa makosa na kwamba hata kama gari limekamilika kwa asilimia 100 askari watatafuta kosa lolote ili mradi tu madereva wakutwe na hatia.

Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu Mkoa wa Kigoma, Frank Makua, anapendekeza sheria iweke wazi juu ya uwapo kwa jengo la pamoja kwa ajili ya polisi, Wakala wa Misitu (TFS) na Halmashauri ili kupunguza vizuizi na urasimu vinavyochangia rushwa kwa sababu anaamini vizuizi vyote vinafanya kazi moja.

Naye mwananchi, Peter Bwenga anasema anachokiona ni maelekezo kutoka mamlaka za juu kwa kuwa jambo hili liko wazi na viongozi wa mkoa wanaona yanayotendeka barabarani na anaamini kwamba wangeamua kufanya jambo kutokomeza 'ushirikiano' wangeweza kwa kuwa serikali haijawahi kushindwa kitu.

Kiongozi wa KIBOTA, jina tunalo, anasema tatizo la rushwa barabarani linasababishwa na usimamizi mbovu wa sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa akitaja namna ambavyo taasisi moja ya haki za binadamu ilivyoanza kuingia barabarani kutafuta haki za binadamu na kisha kuomba pesa kutoka kwa madereva.

"Barabarani hatuongozwi na sheria. Sheria inakuja tu pale dereva anapokosea, hivyo tunaongozwa na hisia za watu. Kuna siku nimeona watu walioijitamblisha kuwa wa haki za binadamu wakidai abiria amenyimwa haki yake kwa kupakata mzigo wake mdogo akiwa ndani ya gari baada ya hapo wakataka tuwape fedha. Yaani kila mtu ameona barabarani ndiyo sehemu ya kuchuma pesa" anasema.

Mfanyabiashara Mwasiti Ramdhani anasema chanzo cha ukiukwaji wa sheria ya usalama barabarani ni njaa kwa matrafiki, akianisha kuwa kuna kipindi wanawaomba madereva wawapitishie maji au chakula na kwamba kuna kipindi wanaomba hata kupewa Sh. 1,000 ilimradi tu wapate pesa ya kukidhi mahitaji yao.

**NANI AWAJIBIKE?**

Wakitoa maoni ya nani awajibike juu ya utekelezaji mbovu wa sheria hizo, Kemon Obedy anasema serikali inapaswa kuwajibika kwakuwa wanaoumia ni wananchi ambao ni walipa kodi wake, hivyo inapaswa kuingilia kati kukomesha suala hilo.

Hamis Shomari anasema mamlaka zote zinazotekeleza masuala ya usalama barabarani zinapaswa kuwajibika kwa kuwa kinachoendelea kwa namna moja au nyingine wao ndio wasababishi wakuu.

Sheila Shaban anasema wananchi wawajibishwe kwa kushindwa kutoa taarifa za rushwa barabarani kwa mamlaka husika na kwamba wananchi ndio wanaolea ugonjwa huo mbaya.

**Itaendelea.....**

HABARI KITAIFA

# Upotevu wa chakula sasa asilimia 30

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema kwa sasa upotevu wa chakula uliopo ni zaidi ya asilimia 30, hivyo kwa kuendelea kutumia mijadala ya wataalamu na kuhakikisha ubora wa bidhaa unapatikana, wataweza kuzuia tatizo hilo na kuuza zaidi.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Suleiman Serera, aliyasema hayo jana katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Wataalamu wa Sayansi na Teknolojia ya Chakula (TAFST), akimwakilisha Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Suleiman Jafo.

"NFRA (Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula) umejenga maghala mengi kwa sababu kuna upotevu mkubwa wa bidhaa zetu baada ya kuzizalisha. Tunazalisha katika wingi, lakini hakuna maeneo ya kuhifadhi.

"Rais Samia Suluhu Hassan, amehakikisha tunakabiliana na upotevu, kwa sasa upotevu tunaona ni zaidi ya asilimia 30 kwa mujibu wa takwimu, kwa hiyo, tukitumia mijadala ya wataalamu na kuhakikisha ubora unapatikana, tutaweza kuzuia na kuuza zaidi," alisema.

Alisema suala la usalama wa chakula duniani linapewa kipaumbele na TAFST kinajumuisha wataalamu waliosomea na kubobea katika eneo hilo.

"Tunapozungumzia usalama wa chakula, hatuzungumzii wingi wa chakula, bali namna ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kuzitumia kama nchi na dunia.

"Binadamu yeyote ili awe alivyo inatokana amekula nini, ndio maana hata chakula tunachokiangalia katika baadhi ya mikoa nchini inayozalisha kwa wingi hususani nafaka utabaini tunalo tatizo bado na wenyewe ni miongoni mwa maeneo yenye shida ya lishe," alisema.

Alisema wanapopima wanabaini kwamba, kuna changamoto ya kujua ni aina gani ya chakula ambacho wanapaswa kula ambacho ni bora.

Alisema suala la usalama wa chakula si la serikali pekee, lazima kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha wakulima wanatoa bidhaa zilizo bora.

"Ili bidhaa zetu ziingie katika masoko ya kitaifa na kimataifa, lazima kuzingatia ubora na ndio maana hapa tunajadili namna serikali itakavyoendelea kuwatumia wataalam kutatua changamoto na kuongeza masoko," alisema.

Kuhusu uuzaji wa vyakula nje, Dk. Serera alisema wameona Nchi za Kusini mwa Afrika, zikiwamo Zambia na Zimbabwe zimekuwa zikinunua bidhaa tani kwa tani.

Alisema wakifanikiwa kuuza zaidi masoko ya kimataifa wataongeza fedha za kigeni, uzalishaji na kuongeza ajira kwa Watanzania wengi zaidi.

Kuhusu uthibiti wa bidhaa zisizo na ubora kuingia nchini, alisema kupitia Shirika la Viwango Nchini (TBS) linasaidia eneo hilo ambapo kwa sasa wana maabara kubwa ya kutosha inayopima sampuli za bidhaa zinazoingia nchini.

Alisema kupitia Tume ya Ushindani Nchini inasaidia ushindani unaofanyika kuzalisha vyakula na bidhaa bora na hata zinazotoka nje zipatikane zenye ushindani kwa ajili ya kutumiwa.

"Inapojitokeza kuna taarifa za bidhaa zisizo bora tunatumia maabara za ndani kupima na tumekuwa tukidhibiti. Tunapobaini hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu huchukuliwa. Tukilinganisha nyuma na sasa tunaona hatua kubwa imefanyika.

"Tunataka maabara zetu zisiwe tu kwa ajili ya Tanzania, tutoe mchango wa kijiografia, zitumike kwa nchi mbalimbali za ukanda wa Afrika Mashariki na zile za SADC," alisema.

Mtaalam wa chakula, mwanasayansi na mteknolojia wa chakula, Nuru Mwasulama, alisema wamekuwa wakitoa elimu kupitia majukwaa mbalimbali kuhakikisha afya ya jamii inalindwa na wananchi hawapati madhara yoyote.

"Ni wajibu wa mtaalamu kutoa elimu popote alipo kuhusiana na kanuni bora za usafi. Viwanda vingi vinavyoandaa chakula huwa na wataalamu.

"Kwa hiyo, siku kama ya leo inatukumbusha wajibu wetu, kuhakikisha tunasimamia kanuni zote zitakazohakikisha uzalishaji chakula bora na salama.

"Joto liwe ambalo halitasababisha vimelea vya magonjwa na vyomvo ninavyotumika vile ambavyo havileti uchafuzi kwenye chakula," alisema.

Alisema hata kama chakula kikiandaliwa vizuri kinapowekwa juani kinaweza kupungua ubora wake.

Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho, Alice Gomezulu, alisema lengo kuu wanaliloliangalia kupitia mkutano huo ni kuhakikisha chakula kinaendelea kuwa salama na bora.

Katibu wa kamati maalum TAFST na mwanachama wa chama hicho, Baraka Mbajije, alisema kupitia mkutano huo, watachambua mambo mbalimbali yaliyojiri na kutoa ushauri mamlaka mbalimbali zinazohusika na usalama na ubora wa chakula.

Alisema hali ya kutoa chakula salama kwa jamii imeendelea kuboreka na uelewa umeongezeka kwa wananchi ambao sasa wanatambua kwa kuanza na usalama na ubora wa bidhaa kabla ya kutumia.

Alisema wamekuwa wakiishauri serikali kuhusu viashiria vyovyote kupitia vyakula vinavyozalishwa nchini na kuingizwa kutoka nje ya nchi vinavyosababisha athari kwa walaji.



Ofisa Utalii Mkuu na Wakala wa Misutu (TFS), Joe Sendwa (kulia), akimueleza jambo mmoja wa wananchi waliotembelea banda lao wakati wa mkutano wa Nishati wa Viongozi wakuu wa Afrika uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni katikati ni ofisa utalii wa misitu, Anna Lawuo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wafungwa, mahabusu kuwekewa vituo vya uandikishaji wapigakura

**Na Lulu George,** TANGA

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kwa mara ya kwanza inaanza uandikishaji wapigakura kwa wafungwa, wanafunzi wa vyuo vya mafunzo na mahabusu kwa kuweka vituo kwenye magereza yote Tanzania Bara na Zanzibar.

Takriban vituo vya uandikishaji 130 vinatarajiwa kuwekwa kwenye magereza ya Tanzania Bara na 10 upande wa Zanzibar.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Ramadhani Kailima, alisema jana alipokuwa akitoa mada kuhusu maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura awamu ya kwanza kwa wadau wa uchaguzi mkoani Tanga.

Kailima alisema kanuni ya 15(2)(C) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari, Tume imeweka utaratibu wa kuwezesha wafungwa, wanafunzi wa kifungo cha chini ya miezi sita na mahabusu kuandikishwa kuwa wapigakura.

"Hatua hii ni kwa mara ya kwanza kufanyika hapa nchini, hivyo niliombe Jeshi la Magereza kutoa ushirikiano pale shughuli husika itakapoanza kufanyika kwenye maeneo hayo," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa kuzingatia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, katika mkoa wa Tanga, tume inatarajia kuandikisha wapigakura wapya 244,805 ikiwa ni ongezeko la asilimia 18.7 ya wapigakura walioko kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura 1,304,235.

Kwa mantiki hiyo, kwa mkoa wa Tanga, tume inatarajia kukamilisha zoezi la uandikishaji kwa wapigakura wapatao 1,549,040.

Akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa INEC, Jaji Jacobs Mwambegele, alisema lengo la kikao hicho ni kupeana taarifa kuhusu hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Tume ili kufanikisha zoezi la uboreshaji wa Daftarai la Kudumu la Wapigakura.

Jaji Mwambegele alisema utekelezaji huo ni takwa la Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024 kifungu cha 16(5) kinachoweka sharti kwa tume kuboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura mara mbili kati ya uchaguzi mkuu uliomalizika na kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea kwa ajili ya uchaguzi mkuu unaofuata.

Alisema mpaka sasa takribani mikoa 25 nchini imeshakamilisha uboreshaji na mchakato huo unaendelea kwa mikoa iliyobaki kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar.

"Kwa hapa Tanga kazi itafanyika kwa siku saba kuanzia Februari 13 hadi Februari 19, mwaka huu, na vituo vitafunguliwa saa 2:00 asubuhi mpaka 12:00 jioni, hivyo tuhamasishe wananchi kujitokeza kuboresha taarifa zao," alisisitiza.

Jaji Mwambegele alisema katika kuhakikisha tume inakwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia, imeboresha mfumo wa uandikishaji ambapo mpigakura aliyepo katika daftari, ataboresha taarifa zake kwa kutumia aina yoyote ya simu ya kiganjani au kompyuta.

"Wanaotumia simu hata kitochi au kiswaswadu wanaweza kutumia namba *152*00# kisha namba 8 na kisha namba 2 halafu 3 na waendelea na maelekezo kwa simu husika," alisema.

Wapigakura 4,369,531 wanatarajiwa kuboresha taarifa zao ambapo 594,494 wanatarajiwa kuondolewa kwenye daftari kwa kukosa sifa za kuendelea kuwapo kwenye daftari, hivyo baada ya uboreshaji, daftari linatarajiwa kuwa na jumla ya wapigakura 34,746,638.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo la Rais kuhusu raia wa kigeni lifanyike kwa vitendo

**KATIKATI** ya wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan alifanya hafla ya kuwapongeza wadau mbalimbali walioshiriki katika uokozi wa watu na mali katika jengo lililoporomoka Kariakoo na kusababisha vifo vya watu kadhaa, uharibifu na upotevu wa mali.

Moja ya mambo ambayo alizungumza katika hotuba yake, mbali na kuwapongeza wadau hao vikiwamo vikosi vya uokoaji na vile vya ulinzi na usalama, ni suala la raia wa kigeni kufanya kazi ndogo ndogo kama vile uchuuzi wa bidhaa ambazo kwa kawaida hufanywa na wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga.

Kwa muda mrefu, raia hao wa kigeni wameonekana katika maeneo mbalimbali kwenye miji mikubwa kama Dar es Saaam ikiwamo, kutembeza bidhaa mitaani. Wengine wamekuwa katika vituo vya mabasi, vijiweni wakiuza karanga, shanga za kimasai na mahindi ya kuchoma jambo ambalo limelalamikiwa na wamachinga bila kupatiwa ufumbuzi hadi Rais alipotoa kauli.

Kutokana na kukithiri kwa jambo hilo ambalo wakati mwingine limesababisha wamachinga kupigana na wachuuzi hao raia wa kigeni, Rais Samia amemwagiza Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, kuhakikisha anakomesha biashara hiyo.

Agizo hilo la Rais Samia ni la kupongezwa kwa sababu kwa kiasi kikubwa litamaliza sintofahamu iliyokuwa imejitokeza na kuonekana kama mfupa mgumu uliomshinda fisi. Viongozi mbalimbali wamekuwa wakiliona suala hilo bila kuchukua hatua hadi Rais alipoingilia kati na kutoa agizo.

Suala hilo limeonekana Kariakoo kwa wachuuzi wa kigeni ambao wengi huja nchini na kupewa vibali vya ukaazi na kazi kama wafanyabiashara au wawekezaji. Baada ya kuvipata, huingia mitaani kufanya uchuuzi wa vitu vidogo kama nguo, vyombo vya ndani, karanga na mahindi ya kuchoma.

Kinachoonekana hapa ni baadhi ya taasisi zilizopewa dhamana ya kufanya kazi mbalimbali kwa niaba ya serikali kushindwa kutimiza wajibu wao. Miongoni mwa taasisi hizo ni Idara ya Uhamiaji ambayo hutoa vibali, mamlaka za serikali za mitaa kwa maana ya halmashauri na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ambayo husajili wawekezaji na shughuli zao. Sasa iweje mtu anatoka nje ya nchi na kuingia Kariakoo kufanya uchuuzi ilhali amekuja kama mwekezaji au mfanyabiashara?


Jibu ni kwamba taasisi hizo zimelala usingizi wa pono kwa kushindwa kufuatilia kama wageni hao walioingia nchini wanafanya shughuli walizojisajili. Pia taasisi hizo zinashuhudia kinachoendelea mitaani lakini zinashindwa kuchukua hatua ikiwamo kujiridhisha kama raia huyo wa kigeni amepata kibali cha kufanya biashara ya kimachinga ikiwamo kuchoma mahindi kando ya barabara na maeneo ya mikusanyiko ya watu.

Agizo hilo la Rais linapaswa kwenda mbali zaidi kwa kufanya ukaguzi kwenye taasisi mbalimbali ambazo zimeajiri raia wa kigeni kufanya kazi zinazoitwa za kitaalamu ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania ambao maelfu kwa maelfu huhitimu kila mwaka na kuishia mitaani wakiwa hawana ajira.

Baadhi ya taasisi zimeajiri watu wa fani za uhandisi, udaktari, uhasibu, ununuzi na ugavi kutoka nje kwa madai kuwa ni wataalamu wakati kazi hizo zinaweza kufanywa na vijana wa Kitanzania ambao kutwa kucha wanalalamika kukosa ajira. Kwa sasa Tanzania kuna vijana waliosomea na kubobea fani kama vile uhasibu na ununuzi lakini hawana ajira huku kazi hizo zikifanywa na raia wa kigeni.

Kwa ujumla, Rais Samia ameonesha njia katika hilo lakini taasisi za serikali zenye dhamana ya masuala ya kazi kama vile Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi Ajira na Vijana) na Ofisi ya Kamishna wa Kazi zinapaswa kuamka na kuanza msako wa raia wa kigeni wanaofanya kazi zinazoweza kufanywa na Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Magari ya shamba ni kero Mbezi Mwisho, trafiki ingilieni kati

Na Sabato Kasika

**KITUO** cha daladala cha Mbezi Mwisho, Dar es Salaam, kinahudumia magari ya abiria yanayotoa huduma katika maeneo mbalimbali ya mkoa, mabasi ya mwendo wa haraka na magari yanayosafirisha abiria kwenda mikoa ya Pwani na Morogoro, ambayo ni maarufu kama 'magari ya shamba'.

Uwapo usafiri wa kutosha ukiwamo wa bajaj katika kituo hicho, unakifanya kiwe na abiria wengi ambao kila siku wanaofika hapo hupata huduma hiyo kuelekea ndani na nje ya Dar es Salaam.

Hata hivyo, kumekuwapo na kero ya muda mrefu inayochangiwa na madereva wa magari ya shamba ambayo inalalamikiwa na baadhi ya madereva wa daladala na abiria wao, lakini haijapatiwa ufumbuzi.

Kero hiyo ni madereva hao kutoka kituoni na kwenda kuyaegesha katikati ya barabara ili kusubiri abiria na kusababisha mengine yanayotaka kutoka kituoni hapo kukosa sehemu ya kupita.

Si alfajiri, asubuhi, mchana wala jioni, bali ni muda wote wanafanya mchezo huo ambao unasababisha abiria wakwame kituoni hapo hata kwa zaidi ya dakika 20 wakisubiri magari hayo yapite.

Magari hayo ya shamba ni kero, ninadhani ipo haja kwa trafiki kuingilia kati kwa kuwadhibiti madereva hao ambao wanakwamisha watu kuwahi katika majukumu yao ya kila siku.

Wenye uwezo wa kumaliza kero hiyo ni wao, wangeangalia uwezekano wa kuweka mtego wa kuwanasa madereva wote wa magari ya shamba wanaotoka kituoni na kwenda kusubiri abiria barabarani.

Mfano, wanaweza kufika kituoni hapo na kujificha ili kuona mchezo mzima unavyofanyika na kisha kuwashughulikia madereva wote wanaokwamisha wenzao kwa kuziba barabara.

Fikiria, mtu anafika kituoni hapo saa 11 alfajiri kwa lengo kuwahi katika mihangaiko yake ya kila siku, anakuta usafiri upo, anapanda lakini daladala haiondoki kwa sababu kuna foleni ya magari ya shamba.

Kwa nini magari hayo yasipakie abiria yakiwa kituoni badala ya kusimama katikati ya barabara? Lengo lao ni nini wanapokwamisha wenzao kusafirisha abiria kwa wakati ili wawahi katika shughuli zao?

Mtindo huo unasababisha baadhi ya madereva wa daladala za kuelekea mjini kulazimika kupita barabara ya mchepuko hadi Mbezi Kwa Yusuph na kupita juu ya daraja ili kuvuka upande wa pili wa barabara na kuendelea na safari ili wasiendelee kukwama kituoni hapo.

Kulazimika kupitia njia hiyo, ni wazi magari ya shamba yanachangia daladala kuchoma mafuta zaidi, kwani daladala yenye ruti ya katikati ya jiji, inalazimika kwenda uelekeo wa Kibamba ndipo igeuze.

Sasa inaonekana kama ni haki yao kuziba barabara na kuanza kusubiri abiria, kwani wakati mwingine wanapoambiwa waondoke, huwa wanakuja juu na hata kutoa matusi ya nguoni.

Kwa kuwa wanaohusika na usalama barabarani wapo, basi ni vyema wafike kituoni hapo wajionee hali halisi na kuona njia bora ya kumaliza kero hiyo isiyo ya lazima wanayokumbana nayo abiria.

Lakini pia kero hiyo inakuwa kubwa zaidi pale watu wanaokusanya ushuru wa shilingi 1,000 ambao nao husubiri daladala zianze kuondoka kituoni na kuzisimamisha ili kondakta alipe kiasi hicho cha fedha.

Hao nao wangepangiwa utaratibu wa kukusanya ushuru ambao si kero kwa abiria na madereva wa daladala, kwani inachosha kuondoka kituoni na kuanza kupanga foleni ya kutozwa Sh. 1,000.

Njia mojawapo ambayo ninadhani wanaweza kuitumia ni kuingia ndani ya daladala na kuchukua ushuru huo kabla hazijaondoka kituoni ili kuepusha usumbufu kwa abiria, ambao umekuwa ukijitokeza.

**MAKALA**

**FIKRA MBADALA**

# Ijue Katiba, nguvu ya Chama na mamlaka ya Mkutano Mkuu CCM



Pascal Mayalla

KWA vile huu ni mwaka wa Uchaguzi, na mimi zaidi ya kuwa mwandishi na mtangazaji wa kujitegemea, pia ni mwanasheria na wakili wa kujitegemea na kwa muda mrefu nimeandika sana kuhusu katiba ya nchi. Kwa hiyo nimeona hakuna ubaya kuwaelimisha watu kuhusu katiba za vyama na kwa kuanzia, kuijua Katiba ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Uchaguzi wa kuanza na katiba ya CCM ni kutoana na kwamba Jumatano ya wiki ijayo (Februari 5) ni siku ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwa CCM. Tuanze na historia ya CCM, ilianzishwa lini na kwa namna gani.

Chama Cha Mapinduzi kilianzishwa kwa azimio la Mkutano Mkuu wa Taifa wa pamoja wa TANU iliyokuwa ikitawala Tanzania Bara tangu kabla ya uhuru wa Tanganyika wa mwaka 1961 na ASP (Afro Shiraz Party iliyoleta ukombozi Zanzibar) kuwa jukumu lao ni kuimarisha umoja, kuleta mapinduzi ya kijamaa Tanzania na kuendeleza mapambano ya ukombozi katika Afrika na duniani kote.

Hiyo ni kwa kuzingatia na kuthamini kazi nzuri ya kimapinduzi iliyokwishafanywa na vyama hivyo, katika kumwondoa Mwafrika kutoka kwenye unyonge wa kunyonywa, kunyanyaswa na kudharauliwa na kumfikisha kwenye uhuru na kuheshimiwa.

Tamko lenyewe la kuiunda CCM ni hili: “Sisi wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa pamoja wa TANU na ASP tuliokutana leo tarehe 21 Januari, 1977 mjini Dar es Salaam, chini ya uongozi wa pamoja wa Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa TANU na Ndugu Aboud Jumbe, Rais wa ASP, kwa kauli moja tunaamua na kutamka rasmi kuvunjwa kwa Tanganyika African National Union (TANU) na Afro Shirazi Party (ASP) ifikapo tarehe 5 Februari 1977 na wakati huo huundwa kwa chama kipya cha pekee na chenye uwezo wa mwisho katika mambo yote kwa mujibu wa Katiba.”

Hivyo CHAMA CHA MAPINDUZI, kwa kifupi CCM kikazaliwa Februari 5, 1977 na makao makuu ya CCM ni Dodoma na Ofisi Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Kisiwandui, Zanzibar na kuna Ofisi Ndogo ya Makao Makuu Lumumba, Dar es Salaam.

Imani za Chama Cha Mapinduzi ni Binadamu wote ni sawa. Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake na Ujamaa na Kujitegemea ndiyo njia pekee ya kujenga jamii ya watu walio sawa na huru.

CCM ina malengo 19 na lengo kuu ni kushinda katika uchaguzi wa serikali kuu na serikali za mitaa Tanzania Bara naZanzibarilikuundana kushika serikali kuu na serikali za mitaa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande mmoja na Zanzibar kwa upande wa pili.

Malengo mengine ni kulinda na kudumisha uhuru wa nchi na raia wake; Kuhimiza ujenzi wa Ujamaa na Kujitegemea kwa mujibu wa Azimio la Arusha;

Kusimamia utekelezaji wa siasa ya CCM pamoja na kuendeleza fikra za viongozi waasisi wa vyama vya TANU na ASP, kama zilivyofafanuliwa katika maandiko mbalimbali ya vyama hivyo; na kuona kwamba kila mtu anayo haki ya kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake na mali yake kwa mujibu wa sheria.

Mengine ni kuona kwamba katika nchi kila mtu aliye na uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi na kazi maana yake ni shughuli yoyote halali inayompatia mtu riziki yake; kusimamia haki na maendeleo ya wakulima, wafanyakazi na wananchi wengine wenye shughuli halali za kujitegemea; na hasa kuona kwamba kila mtu ana haki ya kupata malipo yanayostahili kutokana na kazi yake.

Malengo mengine ni kuona kwamba kwa kutumia vikao vilivyowekwa, raia anayo haki ya kushiriki kwaukamilifukatikakufikia uamuzi wa mambo ya taifa na yanayomhusu, na kwamba anao uhuru wa kutoa mawazo yake, wa kwenda anakotaka, wa kuamini dini anayotaka na kukutana na watu wengine, maadamu havunji sheria au taratibu zilizowekwa.

Pia kuona kwamba nchi inatawaliwa kwa misingi ya kidemokrasia na ya kijamaa; kuhifadhi, kukuza na kudumisha imani na moyo wa kimapinduzi miongoni mwa Watanzania pamoja na ushirikiano na wanamapinduzi wengine kokote waliko; kuweka na kudumisha heshima ya binadamu kwa kufuata barabara kanuni za Tangazo la Dunia la Haki za Binadamu.

Mengine ni kuona kwamba Dola inakuwa Mhimili wa Uchumi wa Taifa; kuona kwamba serikali na vyombo vyote vya umma vinasaidia kwa vitendo kuanzishwa na kuendeleza shughuli za ushirika na za ujamaa, na shughuli nyinginezo halali za Wananchi za kujitegemea; kuona kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya Wananchi na hasa jitihada za kuondosha umasikini, ujinga na maradhi.

**- Wiki ijayo nitaendelea kuhusu uanachama wa CCM, nguvu za mwanachama na nguvu za Mkutano Mkuu wa CCM.**

**Wasalaam.**

**Paskali +255 754 270403**

**KONA YA AFYA**

# Sahani ya lishe bora kwa wagonjwa wa figo



Na Dk. Mabula Budodi

KUTHIBITI ugonjwa sugu wa figo ni changamoto kubwa inayohusu wagonjwa na watoa huduma wa wagonjwa majumbani na hata katika sehemu za afya.

Hiyo inahitaji uelewa na ufuatiliaji wa kitaalamu wa kutumia dawa, chakula na kubadili mfumo wa maisha ili mambo yaende kama inavyopaswa. Kutokufuata mfumo mzuri wa lishe kunaweza kusababisha figo kuharibika zaidi na hata kuleta madhara zaidi.

Bado matibabu ya figo muda mwingine yanaweza kutofautiana na aina ya uharibikaji na ufanyaji kazi wa figo hadi kufikia kuchuja damu, kuondoa maji yaliyozidi mwilini na taka mwili zilizozidi.

Kabla ya mgonjwa wa figo kufanya lishe, ni vyema zaidi kwenda kuonana na daktari na mtaalamu wa lishe kwa pamoja kujua hasa nini zaidi inabidi apunguze na vipi inabidi aachane navyo kabisa ili kupata matokeo mazuri yanayoeleweka.

Si vyema kuchagua aina ya chakula kwa kusikia bila kujua ufanyaji kazi wa figo wa sasa na nini kinahitajika. Lishe hii itategemea zaidi ni kwa namna gani figo zinafanya kazi.

Muda mwingine, kama figo zina uwezo wa kuchuja kwa kiasi kinachotakiwa, mtu huruhusiwa kula chakula bora kama watu wengine wasio na changamoto ya figo.

Wagonjwa wa figo wanatakiwa kufuatilia kiwango cha protini kwenye chakula chao, kiwango cha chumvi, yaani sodium inayopatikana zaidi kwenye chumvi ya kupikia, kiwango cha potasiamu, kiwango cha kalsiamu, kiwango cha fosforasi na hata kiwango cha unywaji maji. Hii ni kutokana na kiwango cha changamoto ya figo kilipofikia.

**PROTINI**

Kwa siku, mgonjwa wa figo huhitaji kilogramu 0.8 ya protini ambacho hupendelewa kitokee zaidi kwenye vyakula vya mimea, lakini huwa tofauti kwa wagonjwa wenye changamoto ya figo inayopoteza protini haitawafanya kuhitaji kiwango cha protini zaidi.

**SODIAMU**

Hii itahitajika gramu mbili kwa siku kwa wanaokuwa na shinikizo la damu, shida ya mwili kujaa maji hata pia kuwa na uwezo wa figo zao kupoteza protini kwa urahisi.

Ulaji wa chumvi kwa wingi huongeza shinikizo la damu maradufu ambayo itasababisha kuharibu figo zaidi na hata kuongeza kiwango cha maji zaidi mwilini.

**POTASIAMU**

Hii kwa wote uhitaji huweka kiwango chao cha potasiamu kinachotakiwa lakini pia hutegemea zaidi kwenye watu wenye usugu zaidi wa matatizo ya figo zao, kiwango cha uharibikaji wa figo zao pia.

**KALSIAMU**

Kupunguza kiwango hiki kiwe chini ya gramu moja kwa siku katika vyakula hata dawa za kunywa pia.

**FOSFORASI**

Hii inapendelewa ipatikane kwenye mboga zaidi na isizidi kiwango cha ulaji kwa siku usiozidi gramu 0.8 hadi moja.

Mifano ya vyakula vya kuepuka kutokana na makundi yenye kiwango kikubwa cha potasiamu, kwa matunda ni parachichi, ndizi, nazi, tikiti aina ya kantalupu, embe, chungwa, tende na matunda ya kukausha ambayo pia yana kiwango maradufu cha potasiamu.

Mboga ni brokori, viazi vitamu na vyeupe, nyanya, karoti mbichi, kabichi mbichi na boga wakati protini ni maharage mekundu na kahawia zaidi, dagaa, nyama nyekundu, samaki wa kamba na salimoni.

Vyakula vya ziada vyenye potasiamu nyingi ni mtindi, maziwa ya soya, tomato sauce, chokoleti, peanut butter, maziwa ya wanyama ya kugandisha na kusindikwa na soda. Vyakula hivi vinapaswa kupunguzwa au kuachwa kutokana na kiwango cha ufanyaji kazi wa figo.

Makundi ya vyakula vyenye kiwango kidogo au stahiki cha potasiamu kutokana na makundi ni matunda ambayo ni zabibu, tufaa au sharubati (juisi) yake tikiti, nanasi, strawberry, raspberry, peach, na beri nyeusi.

Vyakula jamii ya mboga ni bamia, kagaji iliyopikwa, karoti ya kupikwa, alizeti, mahindi, tango, maharage ya kijani, mbaazi, vitunguu na spinachi. Protini ni korosho, kuku, mayai, mbegu za maboga, mbegu za alizeti, almondi, karanga na jozi/walnuts wakati wanga ni mahindi, ngano, mtama, uwele na mchele.

Makundi hayo ni vyakula kwa watu wenye changamoto ya figo ambao wanatakiwa kuonana na watalamu wa afya na watalamu wa lishe kwa ufanisi wa lishe.

**- Dk. Budodi ni daktari wa tiba ya binadamu anapatikana Dar es Salaam. Unaweza kuwasiliana naye kwa simu Na. 0710980096 au baruapepe mabulabudodi@gmail.com**

RIPOTI MAALUM – 3

# Mikakati ya kudumu kudhibiti utiririshaji tope kinyesi nyakati za mvua jijini Mwanza

**Vitus Audax,** MWANZA

**KATIKA toleo lililopita zilibainishwa sababu kuu zinazofanya tatizo la utiririshaji majitaka kutoka katika vyoo vya watu waishio milimani nyakati za mvua. Sehemu hii inaonesha juhudi na hatua zinazochukuliwa ili kudhibiti tatizo hilo.**

HALI ya utiririshaji wa majitaka, utapishaji vyoo katika njia zisizo salama pamoja na milipuko ya magonjwa, vinatishia uhai wa watu kinyume cha Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, inayompa kila mtu haki ya kuishi kwa mujibu wa sheria.

Kadhalika Ibara ya 26(1) inamtaka kila mtu kuwajibika katika kufuata na kutii Katiba na sheria za Jamhuri ya Muungano.

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura Na. 191 inatambua haki ya raia wote kuwa na mazingira safi na salama. Katika muktadha huu, usimamizi salama wa majitaka ni muhimu kwa faida ya umma kwa ujumla na ni haki ya kila mwananchi.

Baadhi ya wananchi na wakazi wa maeneo ya milimani na tambarare jijini Mwanza wanasema kutokana na utiririshaji wa topekinyesi katika makazi ya watu na vyanzo vya maji kwa siku za mvua, wanaiomba serikali kuchukua hatua za haraka katika kudhibiti, kuelimisha jamii na kutengeneza miundombinu imara itakayosaidia kudhibiti tatizo.

Juliana Elias, mkazi wa Mabatini anasema utaratibu wa kusimamia na kukagua vyoo uzingatie vigezo ikiwa ni pamoja na kuwatoza faini wote wenye vyoo duni na kutoa onyo kali kwa wanaotiririsha majitaka hayo katika makazi ya watu.

Aidha anasema mabibi na mabwana afya katika maeneo husika wamezoeleka hivyo kupunguza ufuatiliaji juu ya watu wa namna hiyo huku wakiwa na kisingizio kuwa wanafanya hivyo kwa uficho.

Mkazi wa Ghana, Aman Kyasekile, anasema jambo hilo ili likomeshwe, wananchi wenyewe wanatakiwa kuwa na uelewa kisha kuwa walinzi wa kila mmoja na kuhakikisha kila mwenye utaratibu wa kutiririsha taka hizo wanatoa taarifa ili achukuliwe hatua.

"Serikali wanaweza kuanza na jamii husika kwani wenyewe ndio chanzo cha uchafuzi huu pia iweke miundombinu kwa ajili ya kusaidia wananchi wasichafue mazingira,"anasema Kyasekile.

Mariam Hussein Mkazi wa Kilimahewa anasema elimu kwa wananchi bado ni tatizo hivyo ipo haja ya serikali kupitia wataalam wake kuhakikisha elimu inatolewa katika ngazi za mitaa na vitongoji lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanatambua madhara na kuacha.



Maji machafu yenye kinyesi yakitiririshwa katika mtaro. **PICHA:MTANDAO**

Mkazi wa Kirumba, Abdul Khasim anasema katika maeneo ambayo magari hayawezi kufika basi serikali iweke miundombinu ya uondoshaji majitaka.

"Wanatumia njia hizo kwa kipindi cha mvua kutokana na magari kutokuwafikia. Hivyo ni vyema wawekewe miundombinu salama kama chemba zilizopo mjini kati. Miundombinu hiyo itasaidia kuchukua taka moja kwa moja, pia hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao watakaoendelea kukaidi,"anasema Khasim

Bahati Ally, mkazi wa Mtaa wa Nyerere Mabatini, anasema sehemu kubwa ya hatua zimechukuliwa katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na wananchi kutozwa faini lakini bado hali hiyo inaendelea, hivyo kuomba serikali kuja na mpango mbadala kunusuru wananchi wa maeneo hayo.

**MIKAKATI YASUKWA**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Mazingira wa Jiji la Mwanza, Desderius Polle, anasema miongoni mwa mikakati ya jiji baada ya kuona tatizo hilo linadumu kwa muda mrefu, kwa kushirikiana na mamlaka zingine wanahakikiti watoa elimu kwanza kwa jamii kisha kuchukua hatua za kisheria.

Anasema mkakati wa muda mrefu ni kutoa elimu juu ya ujenzi wa vyoo vya kisasa, kutumia chemba zinazotengenezwa na mamlaka husika na kuacha utiririsha wa maji taka hayo sambamba na kuwatahadharisha juu ya kuwa kufanya hivyo ni ukiukwaji wa sheria na taratibu zilizowekwa kwa ajili ya usimamizi wa mazingira.

"Eneo kubwa la Mwanza mjini tayari umewekwa mfumo wa uondoshaji majitaka vilevile sehemu ya maeneo ya Igogo. Baadhi ya maeneo ya Mabatini na Bugalika wamewekwa pia mabalozi wanaosimamia mfumo huo ili inapotokea shida ya kuziba, wanawahi kwa ajili ya kuzibua,"anasema.

Mbali na hatua hizo, anasema wako katika mpango mkakati wa muda mrefu wa kuvipatia elimu pamoja na vifaa vya kisasa vikundi vinavyozibua vyoo ili kuondosha taka hizo katika hali ya usalama bila kuharibu mazingira na kuhatarisha afya za wananchi.

Anasema kutokana na hali ya miundombinu kutokufikika wanatarajia kuwapatia wanavikundi hao, maarufu kama Tobazi, pikipiki za mizigo (maguta) zenye matangi, mashine kwa ajili ya kuondosha majitaka kwenye chemba ili kufika katika maeneo ya wakazi wa milimani kwa urahisi.

Mpango huo, anasema utakuwa suluhu kutokana na uwezo wa pikipiki hizo kufikia sehemu kubwa ya nyumba za wakazi waishio milimani na kutoa huduma hiyo katika hali ya usalama.

Pia anasema maji hayo yote yakikusanywa yanapelekwa kwenye mabwawa maalum ya Butuja wilayani Ilemela kwa ajili ya kutibiwa kabla ya kuruhusiwa kutiririshwa ndani ya Ziwa Victoria.

Ofisa Afya wa Jiji la Mwanza, Audiphace Sabbo, anasema katika mikakati ya muda wote halmashauri imekuwa na utaratibu wa kutuma timu ya wilaya ambayo inaenda ngazi ya kata hadi mtaa kutoa elimu ikishirikisha maofisa afya wa kata, kamati za afya ngazi ya kata, mtaa, mhudumu wa afya ngazi ya mtaa pamoja na uongozi wa serikali za mitaa kwa maana ya wenyeviti.

"Ushirikishwaji huu unatusaidia kufikisha ujumbe wa afya kwa jamii husika ambako, tunaandaa mikutano mara nyingi suala la vyoo bado tatizo kutokana na kujenga vyoo vya muda ambavyo ni sehemu kubwa ya madhara hivyo elimu ni endelevu,"anasema.

Kadhalika, anasema wanafanya ufuatiliaji katika maeneo yanayoshukiwa kuwa na magonjwa ya mlipuko na kuhakikisha wanachukuliwa wahisiwa na kupatiwa matibabu.

Anasema katika kudhibiti matumizi ya maji machafu halmashauri imekuwa ikitumia vidonge vya kutibu maji ili kuzuia kuibuka kwa magonjwa. Anasema hatua hiyo ni msaada kwa asilimia kubwa kutokana na baadhi ya watu kutumia zaidi maji ya visima.

"Tunashauri maji yachemshwe, yakipoa jamii inapewa vidonge ambavyo matumizi yake ni kidonge kimoja kwa lita nane hadi 10. Vidonge vinatolewa kulingana na idadi ya watu kwenye kaya na hii imetusaidia sana kwani kwa mwaka wa fedha 2024/25 hatujapata wagonjwa wa kipindupindu," anasema.

**HATUA ZA KISHERIA**

Sabbo anasema sheria haziko kimya kuhusu suala hilo na kuwa ni kazi ya kila siku ya maofisa afya ngazi ya kata na mitaa kukagua maeneo yote ya makazi, biashara na taasisi kama vyuo, shule na maeneo ya ibada kama wana vyoo bora na usafi wa kaya. Wakikuta kuna upungufu, wanatoa siku ili wafanyie marekebisho lakini wakishindwa wanachukuliwa hatua ikiwemo faini na kushtakiwa.

"Lengo si adhabu lakini mtu akiendelea kukaidi inabidi apatiwe adhabu ikiwamo faini kulingana na Sheria ya Halmashauri ya Jiji ya mwaka 2017 isiyozidi Sh. 50,000. Faini nyingine ni kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Jamii ambayo kiwango chake ni kuanzia Sh.500,000 mpaka milioni moja," anasema.

Kwa ngazi za mitaa, anasema ziko kamati za afya ambazo zimejiwekea sheria ndogondogo zinazotumika kuhakikisha wanatoa adhabu pindi wanapobaini vitendo vya aina hiyo wakati wa kuzungukia mitaa yao.

Anasema ikishindikana huko, mtaa husika unapeleka mtu huyo ngazi ya baraza la kata ambapo ikishindikana katika ngazi hiyo, ofisa afya analazimika kupeleka shauri hilo kwa Mwanasheria wa Halmashauri ambaye anawajibika kumfungulia kesi mtu huyo mahakamani.

**WADAU WAJITOSA**

Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira kutoka MWAUWASA, Mhandisi Salim Lossindilo, anasema serikali kupitia mamlaka hiyo inaendelea kutafuta wadau kwa ajili ya kushirikiana nao katika kutekeleza miradi ya mfumo ya ondoshaji maji taka katika vyoo vya wananchi 'simplified sewerage system'.

Anasema katika mwendelezo wa kuweka mifumo hiyo ya kudhibiti tatizo hilo tayari mamlaka hiyo imetia saini mkataba Novemba 23, 2022 wenye thamani ya Sh. bilioni 12.7 kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya majitaka katika maeneo ya Ilemela na Jiji la Mwanza unaotarajiwa kuziunganisha kaya 1,600.

Anasema taratibu za utekelezaji wa mradi huo unaodhaminiwa na wadau wa maendeleo kutoka Umoja wa Ulaya pamoja na Serikali ya Ujerumani na kutekelezwa kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria Afrika Mashariki zinaendelea na kuwa kufikia Mwaka 2026 unatarajiwa kuwa umekamilika.

Mhandisi Lossindilo anataja maeneo yatakayofikiwa na Mradi huo kuwa ni pamoja na sehemu ya Kata ya Kirumba, Pasiansi, Kitangiri, Nyamanoro, Igogo pamoja na maeneo ya milimani Ilemela.

Mhandisi Mkuu na Mratibu wa Miradi inayotekelezwa kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria kutoka Wizara ya Maji, Mhandisi Abdullah Matata, anasema mradi huo ni miongoni mwa miradi inayoratibiwa katika maeneo ya Kisumu nchini Kenya,Kigali ya Rwanda,Kampala ya Uganda pamoja na Burundi.

"Wito wangu ni kwamba wananchi wahamasike kulinda miundombinu itakayojengwa ili iendelee kutoa huduma ipasavyo lakini pia wahakikishe wanafuata utaratibu rafiki utakaowekwa na MWAUWASA wa kuwezesha wananchi kuunganishwa kwenye mradi," anasema Mhandisi Matata.

# MAISHA

FEBRUARI 2, 2025
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 13

**Rayon pajama ya vijana**



Ukurasa 15


**MAISHA NI NYUMBA**

Hizi ndizo njia za kukabiliana na majanga ya moto kwenye nyumba



Ukurasa 12

**HARUSI**





## Epuka kufanya haya unapotafuta urembo

Ukurasa 14

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | ■ | N | G | A | N | O |
| A | ■ | ■ | ■ | G | ■ | N |
| J | ■ | T | I | A | ■ | G |
| A | R | A | ■ | N | A | O |
| N | ■ | M | T | O | ■ | P |
| G | ■ | B | ■ | ■ | ■ | E |
| A | G | A | N | A | ■ | A |


## FUMBO TOTO

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


MBU, BUU, GUU, GOA, BAMBA, NDUGU, TANGA, IBAKI, PANGANI, ANGUKIA



## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

TUMEPOTEA ZIWANI, SASA TUPANDE MTUMBWI KUFIKIA LANGO KUU LA MJI.



## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO John alikuwa na kawaida ya kwenda mtoni kuoga peke yake. Siku moja akiwa njiani alikutana na bibi mmoja akiwa anaokota kundi kando ya barabara akiwa peke yake.

John alimuhurumia yule bibi na kuanza kumuuliza

**John:** bibi shikamoo

**Bibi:** Marhabaa mjukuu wangu

**John:** Mbona unaokota kuni katika pori hili peke yako, wajukuu zako wako wapi wakusaidie?

**Bibi:** Mjukuu wangu niko hapa porini peke yangu, kama wewe unavyokwenda mtoni ukiwa peke yako

**John:** Ulijuaje bibi kama naenda mtoni kuoga?

**Bibi:** Nimejua kama wewe ulivyojua naokota kuni hapa, lakini sisi wote tunafanya vitendo vya hatari

John alishtuka na kuangalia nguo zake alizoweka begani, kisha akakimbia kurudi nyumbani

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Uovu nyumba za baba zetu unavyotesa wengi!

***KARIBU tena msomaji wangu tudadavue pamoja maisha yalivyo. Wiki mbili zilizopita tulichambua habari ya ndoto nikasema ndoto zako unazoota usiku zinaweza kufutwa na maadui wasiokutakia mema.***

Ndoto ni kile kitu ambacho Mungu amekupa kukifanya duniani, lakini adui anakipindisha ili usifanikiwe. Nilitaja baadhi ya vifutio vya ndoto. Mfano, unapoota ndoto unalishwa chakula hiyo ni kifutio cha ndoto.

Kifutio cha pili unatishiwa kwenye ndoto. Unaota ndoto nzuri lakini inapochanganyika na ya vitisho, ile nzuri huikumbuki bali unakumbuka ile ya vitisho. Na tatu, ni kuota ndoto unafanya zinaa, yaani unazini kwenye ndoto.

Leo tuangalie eneo lingine kuhusu kile kilichojificha kwenye nyumba ya baba yako, kinavyoweza kukutesa pasipo kujua. Ipo nguvu ambayo inafanya ukatili wa hali ya juu kwenye maisha ya watu.

Lakini hiyo nguvu imejificha kwenye nyumba za baba zetu. Kwa mfano, Adamu, mwanadamu wa kwanza alipolaaniwa na Mungu, hiyo tayari ilikuwa ni uovu ambao uliachiliwa juu ya maisha yake.

Lakini alipotoka mbele za BWANA alionekana kawaida. Ila ule uovu uliendelea kujificha ukaja kufanya kazi kwa watoto wake, Kaini akainuka ghafla akamkamata ndugu yake Habili akamuua.

Mungu alitamka laana ikaishia pale. Lakini kumbe ile mbegu ilikuwa inachipua ndani. Yaani Adamu alipopata watoto hakuelewa nini kinachoendelea.

Lakini pia utaona kuwa moja ya uovu uliojificha unaofanya ukatili mkubwa sana wa viwango vya juu ni nguvu za laana zilizoachiliwa kwenye nyumba za baba zetu.

Unaweza kuwa unaona vitu haviendi, unapambana kimaisha lakini ni kama vile unaenda mbele kisha unarudi nyuma. Kumbe kuna nguvu ya laana ilishatamkwa ama kwenye ardhi au kwenye nyumba ya baba yako.

Kuanzia ukoo ulikotokea yaani nyumba ya babu mzaa babu. Kumbuka nguvu ya uovu inaitwa laana na unaweza kudumu kwenye maisha ya mtu kwa zaidi ya miaka 400.

Yaani miaka yote hiyo ule uovu umejificha halafu unakuja kuibuka. Mfano mtu mmoja kwenye maandiko ya Mungu, Joshua alitamka maneno juu ya Yeriko.

Akasema huu mji wa Yeriko mtu atakayejenga msingi atafiwa na mtoto wake wa kwanza na atakayesimamisha malango yake kwa kufiliwa na mtoto wake mwanamume aliye mdogo. Na hiyo ilikuja kutokea. (Yoshua 6:26).

Baada ya Yoshua kutamka ilipita miaka takriban 500 maneno yake yakatimia. (1Wafalme 16:34). Huo ndio uovu uliojificha ambao unakuja kufanya kazi wakati ambapo mtu hajui chochote kinachoendelea.

Huu uovu umejificha kwenye nyumba ya baba. Ukiangalia pale Yoabu anatamkiwa neno gumu sana anaambiwa hii damu ya Abuneri itakuwa juu ya kichwa chake Yoabu, lakini na nyumba ya baba yake.

Uovu uliojificha kwenye nyumba ya baba yako ndio ulio mbaya sana kuliko ule uovu ambao unaweza ukauzungumzia wewe.

Watu wengi leo wanateseka na wapo kwenye ukatili mbaya sana kwa sababu ya uovu uliojificha kwenye nyumba za baba zao! Yale ya kwako unagundua ulishamaliza wewe na Mungu.

Lakini ule uovu ambao haujawahi kushughulikiwa ambao upo kwenye nyumba ya baba yako, huo ndio unaosababisha mabaya ya siku zote.

Lipo andiko la Mungu linasema, "Baba zetu walitenda dhambi hata hawako; Nasi tumeyachukua maovu yao", (Maombolezo 5:7) Leo unapambana, mbona maisha hayaendi, unajiuliza maswali, kila mahali nafeli. Mbona namtumikia Mungu vizuri. Lakini kumbe umesahau kushughulika na uovu unaofanya kazi kwenye nyumba ya baba yako.

> **"Kuanzia ukoo ulikotokea yaani nyumba ya babu mzaa babu. Kumbuka nguvu ya uovu inaitwa laana na unaweza kudumu kwenye maisha ya mtu kwa zaidi ya miaka 400.**

Unaweza kuona kila mwaka kuna mambo yanayofanyika kwenye nyumba ya baba yako ili kutia nguvu ule uovu! Wanaenda kutambika wanafanya vitu vya ajabu.

Unajiuliza mbona nafanya hivi na vile sijielewi. Vitu vinatokea unashangaa kumbe ni uovu uliojificha kwenye nyumba ya baba yako. Fanya maombi ya kuvunja uovu uliojificha kwenye hiyo nyumba ya baba yako.

Kumbuka, moja kati ya ukatili mbaya unaofanya uharibifu kwenye maisha ya watu siyo kile ambacho kipo kwa wakati ule kwa sababu walishaondolewa, wamekufa.

Mpenzi msomaji, bila shaka umepata picha kuhusu kilichojificha kwenye nyumba ya baba yako. Wiki ijayo tutaendelea kuhusu maagano au sheria zinazotutesa. Sheria kwenye familia zetu zinatofautiana, hazifanani.

***Je, una maoni au ushauri? Ujumbe mfupi 0715268581. Namba ipo WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Ruhusu wabaya waondoke, sogea hatua unayoitaka

MAISHA yako yana nguvu zaidi unapojifunza kuishi kwa sasa badala ya kung'ang'ania yaliyopita au kuahirisha furaha yako kwa kesho isiyo ya uhakika.

Kila siku ni fursa mpya ya kujijenga, kujifunza na kustawi. Usiruhusu jana ikufunge au kesho ikupotezee leo.

Binafsi, nimeshawahi kupoteza vitu ambavyo niliamini bila kuwa navyo sitaweza kuishi vizuri.

Nimeshawahi kupoteza watu, ambao niliamini bila kuwa nao sitaweza kufika ninakokwenda. Pia nimeshawahi kupoteza nafasi ambazo niliamini nikizikosa sitaweza kutimiza malengo yangu tena.

Kuna wakati unafika katika maisha unajiaminisha moyoni au unaaminishwa na wanaokuzunguka kuwa bila mtu fulani au kitu fulani basi utakuwa mwisho wa safari yako.

Katika nyakati kama hizo hizo, niliwahi kupewa neno la hekima ambalo limekuwa msaada mkubwa sana siku zote za maisha yangu.

Niliambiwa kuwa si kila unayempoteza au kila unachopoteza ni hasara kwako. Ukiambiwa neno hili katikati ya maumivu hauwezi kuelewa lakini baada ya muda nimegundua lina ukweli ndani yake.

Kuna mabadiliko lazima yatokee kwanza ili uwe vile unavyotaka. Kuna watu ambao ni lazima waondoke kwenye maisha yako ndipo usogee hatua unayoitaka.

Historia ina tabia; na haijawahi kujificha. Kuna wengine inalazimika wapoteze kazi zao za sasa ili wapate kazi kubwa zaidi.

Kuna wengine, inalazimika wakataliwe kwenye mambo fulani fulani ili wapate hasira ya kufanya kitu wanachotakiwa kufanya. Kuna wakati mtu unakuwa umejiachia na hautaki kusumbuliwa kwa namna yoyote.

Mungu anapokuangalia, anajua ukiendelea hivyo hautakuwa vile unatakiwa kuwa; na hautafika kule unatakiwa kufika. Kwa hiyo, ni lazima meli ipitie dhoruba, ili utupwe baharini na umezwe na samaki kisha akakutapike unakotakiwa kwenda.

Si kila dhoruba inapokujia, ukimwomba Mungu ataiondoa, nyingine ameileta ili akutenge na baadhi ya vitu, akutoe katikati ya watu fulani au akutoe kwa lazima eneo, ambalo ukiendelea kuwepo utadumaa na utashindwa kufikia kilele cha mafanikio yako.

Ngoja nikuambie, Mwombe sana Mungu, akili yako ifunguke na using'ang'anie watu ambao unatakiwa kuachana nao.

Kwa nini watu wema wanapatwa na mambo mabaya? Ni kawaida kwa watu wanaosadikiwa kuwa waovu kuonekana wanafanikiwa kuliko wema na waadilifu.

Haya yanatokea ili kuwasidia wema waache kujisahau kwamba hapa duniani ni wapitaji, na wasafiri. Kila kitu kimevurugwa, hata ukifuata sheria utavurugwa na wasiozifuata.

Kwamba kikubwa ni kuomba msaada kwa Mungu pale mabaya yanapokupata; hata kama hayana sababu. Usipoteze muda kulialia kwa nini mimi, kwa nini mimi!

Ukiona mtu anatumia nguvu kubwa sana, kukuchafua kutaka uharibikiwe kimaisha na kukuondoa katika eneo ulilopo, usishangae!

Wewe elewa kwamba huyo ni miongoni mwa wale wanaotegemea kuishi ndoto au maono ya wengine.

Kufanya hivyo, anadhani kwamba yeye ndiyo anastahili kuwepo katika nafasi uliyonayo,ni wale wanaotamani mafanikio ya wenzao badala ya kuvutiwa nayo.

Ikitokea umekutana na mtu wa namna hii, usigombane naye, wala usimchukie, tambua siku zote kwamba, mtu wa namna hiyo yupo gizani na wewe ni nuru.

Hakuna namna hata mara moja, giza likaizidi nuru, endelea kusimamia unachoamini na hasa ukimtambua aliyekubebesha maono hayo ni Mungu na hivyo yatatimia tu. Ni suala la muda.

Walimwengu wanasemaga, wakati ukifika huwa hauna makengeza, na aliyekusudiwa kwa wakati ule atakuwa tu, na asiyekusudiwa kwa wakati husika hatakuwa.

Kama ndivyo! basi ni muhimu tuheshimu nyakati za watu, ili na wewe ujenge nafasi ya kuheshimiwa wakati wa nyakati zako.

Unanisikia au niongeze sauti! usihusudu, wala kuingiwa na tamaa na nyakati za watu. Jenga tabia ya kuheshimu nyakati za watu, kwa sababu nyakati huzunguka.

Pale mahali hazina yako ilipo, ndiko moyo wako ulipo. Kuna uhusiano mkubwa kati ya haya nayoyasema na mahusiano yako na Mungu.

Usitangaze ndoto yako, tangaza matokeo, vinginevyo utaishia kuuzwa utumwani kama Yusufu. Yusuph akaota ndoto, akawapa ndugu zake habari, nao wakazidi kumchukia.

***• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# SEND OFF




**Haikuwa rahisi, hatimaye Thomas na Esther wamefanikiwa kuvuka vikwazo na kufunga ndoa takatifu hivi karibuni na kuwa kumbukumbu nzuri kwao. PICHA: MC GaraB**

## MITINDO



# Rayon pajama ya vijana



SUTI anayovaa Rais Samia Suluhu Hassan, maarufu kama Suti ya Mama Samia ni moja ya vazi linalozidi kupendwa nchini huku likipigiwa chapuo na wasanii na watu maarufu ambao wamejitokeza wakiwa wamevaa.

Hivi karibuni kumekuwa na kampeni ya kulitangaza vazi hilo, huku wasanii mbalimbali wanawake wakionekana wamevaa suti hiyo ikiwa na rangi tofauti.

Suti ya Mama Samia ambayo imetengenezwa kwa koti refu lenye vifungo mbele na kuambatana na suruali ndefu ni mtindo unaohifadhi heshima, unaovutia na wa kipekee pale mtu anapovaa kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Kupata umaarufu wa vazi hilo, linaleta shauku kwa wanawake wengi kwenda kununua au kushona ili angalau kuwa miongoni mwa wanaovaa.

Kimsingi suti hiyo inatumia vitambaa vya aina mbalimbali kama vitenge, Hariri, Khaki au Bazee na ni chaguo la mtu husika kitambaa gani anachopenda.



UREMBO
Na Mary Geofrey



# Epuka kufanya haya unapotafuta urembo

KATIKA harakati za mwanamke kutafuta urembo unaweza kupitia mambo kadhaa ambayo kwa wakati huo utaona yana afya, lakini baadae unakuletea madhara.

Kimsingi unatakiwa kuepuka kufanya vitu ambavyo vinaweza kukuletea athari ya kudumu.

**Tattoo**

Tattoo ni alama ya kudumu kwenye ngozi yako. Inatoa ngozi ya asili jambo ambalo husababisha maambukizi na matatizo mengine, ikiwa ni pamoja na athari za mzio.

Rangi za tattoo hasa za kijani, bluu, nyekundu na njano zinaweza kusababisha athari ya ngozi, kama vile upele unaowasha kwenye tovuti ya tattoo.

Idadi ya tattoo mtu anazochora inahusishwa na hatari ya kuongezeka Hepatitis C, ambayo inaweza kusababisha ugonjwa wa cirrhosis, saratani ya ini, na kushindwa kwa ini. Hasa ikiwa sindano iliyotumiwa kuunda tattoo yako imeambukizwa na damu iliyoambukizwa.

**'Botox'**

Botox hutumiwa kupunguza kuonekana kwa makunyanzi kwenye uso. Inapaswa kutumika tu chini ya usimamizi wa daktari. Sindano lazima ziwekwe kwa usahihi ili kuzuia athari mbaya katika siku zijazo.

Tiba ya Botox inaweza kuwa hatari ikiwa inasimamiwa vibaya. Lenzi za mguso zinazopanua macho yako lenzi za mawasiliano, ambazo hutumika kupanua macho yako, zinaweza kusababisha matatizo ya kuona.

Ukosefu wa udhibiti wa ubora unaweza kusababisha matatizo kuanzia kuwashwa kidogo hadi maambukizi ya kusababisha upofu.

**'Creams' za kupausha**

Mafuta ya 'blekning' ya ngozi yana viwango vya juu vya zebaki. Inatumika katika krimu za kung'arisha ngozi kwa sababu huzuia uzalishwaji wa melanin ya rangi ya ngozi.

Zebaki ina athari mbaya kiafya,inasababisha uharibifu wa figo na uharibifu wa mfumo wa neva.

Ukiona maneno kama vile calomel, mercurous chloride, Mercurio, mercuric, au mercury, tafadhali acha kutumia bidhaa hiyo papo hapo.

MAPISHI

# Supu ya maboga



LICHA ya boga kuwa chakula kitamu sana na majani yake kama mboga pendwa katika familia nyingi nchini, lakini wengi hawajui kama kuna supu inayotokana na boga.

Leo nataka nikueleze namna ya kuandaa supu ya maboga ambayo ni tamu na pia ni rahisi kuandaa.

**Mahitaji**

Kipande cha boga, karoti tatu zikatekate, kitunguu maji kimoja, menya na katakata, chumvi kwa kiasi upendacho, mafuta ya kula kijiko kimoja cha mezani na maziwa freshi nusu lita ambayo utayapasha moto kabla ya matumizi.

Mahitaji mengine ni gharam masala kijiko kimoja cha chai, pilipili kidogo yaweza kuwa pilipili manga nusu kijiko cha chai.

**Jinsi ya kuandaa**

Kwanza menya boga na kuondoa mbegu zote kisha ulikate kate vipande vidogo vidogo. Ziweke pembeni zile mbegu usitupe zichambue kisha osha na uzianike zinafaa kwa matumizi mengine.

Sasa andaa vitunguu na karoti. Vitunguu andaa kama kawaida ambavyo ungefanya kwa matumizi mengine, karoti zimenye na kuzikatakata.

Weka chombo katika moto na uweke mafuta ya kula pamoja na vitunguu, ivisha kidogo tu vitunguu kisha weka karoti, gharam masala, chumvi na pilipili kidogo kama ni mtumiaji.

Ivisha kidogo kisha weka maboga na maji kidogo wacha vichemke pamoja kwa kama dakika saba hadi 10 maji yawe yamepungua kidogo tu kama ikibidi uongeze maji basi ongeza maziwa.

Vinapokuwa vimelainika vizuri na maji yamepungua basi weka kando na uanze kukanda kwa mwiko au kwa kutumia mashine ya kupondea (blender), wakati wa kuponda ponda kama ikiwa na ugumu.

Ongeza maziwa ili kufikia kiwango cha ulaini ukipendacho. Baada ya hapo ni tayari kwa kula na waweza enjoy supu yako na kipande cha mkate.

## MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

# Valentine na pambo pambe lisilosahaulika

TUMEINGIA mwezi wa mapendo. Mwezi wa wapendanao, wa kuonesha thamani ya uhusiano wako na mwezi wako au yule umpendaye sana. Februari mwezi wa Valentine.

Kwanza kabisa, ni lazima uzingatie rangi. Pamoja na kwamba Valentine inatawalia na nyekundu na nyeupe, unaweza kuchanganya rangi nyingine kama pinki, dhahabu au fedha ili kuboresha mwonekano.

Pili, aina ya pambo. Unaweza kuweka 'trei' yenye mishumaa ya ukubwa tofauti, yaani mikubwa kwa midogo, maua na picha yenye ujumbe mahsusi wa mahaba kama 'furaha yangu', 'kila kitu changu', 'hugs and kisses', ujumbe ulioandikwa kwa mkono, picha yenu ya zamani na maneno mengine ambayo yataonesha thamani ya upendo wako.

Kadhalika, mito ya makochi au kitandani, inaweza kuonesha uzito wa upendo kwa kununua ile yenye ujumbe mahsusi, kama nilivyoeleza hapo juu.

Siku hii ni muhimu sana kupata mlo pamoja walau mchana au usiku kama haitawezekana kuwa pamoja siku nzima kutokana na majukumu ya kikazi.

Wataalamu wanaeleza kuwa 'mchawi' wa siku hii ni chakula. Hivyo, kula pamoja kama wapendanao, inaongeza kumbukumbu nzuri kwenye uhusiano wenu.

Kama mtakula pamoja nyumbani, maandalizi ya meza ya chakula ni muhimu kwa kuwa ndiyo kitovu cha sherehe.

"Ni zaidi ya mahali pa kula chakula, kwa siku ya Wapendanao, meza iliyowekwa vizuri ni barua ya upendo isiyofutika inayotengeneza mazingira ya karibu ambayo yanakamilisha hisia za Valentine," anasema Monica Joseph, mtaalamu wa mapambo.



Na Elizabeth Zaya



# Hizi ndizo njia za kukabiliana na majanga ya moto kwenye nyumba

USALAMA wa nyumba ndio jambo la msingi kuliko vyote katika ustawi wake.

Mbali na vitu vingine ambavyo ni muhimu katika nyumba kuanzia maandalizi, wakati wa ujenzi na baada ya ujenzi ni pamoja na kuweka mfumo mzuri wa kuepusha majanga ya moto. Kukosekana kwa mambo hayo, kumesababisha vilio kwa watu wengi hasa yanapotokea majanga kama hayo.

Msanifu Majengo, Eliud Jumanne, anasema ziko njia mbalimbali za kutumia kukabiliana na majanga ya moto kwenye nyumba na mojawapo ni kutumia mfumo bora wa umeme.

Njia ya pili, anasema ni kutumia vizuri soketi na swichi za umeme pamoja na kuepuka kutumia vifaa vya umeme duni vikiwamo redio, pasi, jokofu, televisheni na jiko.

"Kutokana na ujenzi duni, si jambo la kustaajabisha kukuta nyumba moja ina soketi moja au mbili. Hili husababisha watu kujaza kila kifaa kwenye soketi hiyo moja na kusababisha izidiwe na kuwaka moto," anasema.

Ya tatu anasema ni kutumia vema jiko lililoko ndani ya nyumba.

"Jiko lililoko ndani ya nyumba unatakiwa kuchukua tahadhari zaidi. Haijalishi ni jiko la umeme, gesi au mafuta bali unatakiwa kuzingatia mambo ili kuepuka majanga ya moto. Mambo hayo ni kulisafisha, usiliache likiwa na mafuta au kuacha karatasi karibu nalo," anasisitiza.

Njia ya nne anasema ni kuepuka kuacha moto ukiwaka karibu na nyumba. Anashauri pia kutumia moto ulio wazi kwa uangalifu na kwamba wakati mwingine watu huwasha vibatari, mishumaa au hata sigara ndani ya nyumba.

Mtaalamu huyo anasema ni vyema kuandaa miundombinu na vitu vya kukabiliana na moto.

"Ni vyema kuchukua tahadhari kabla ya janga kutokea, ni muhimu ukahakikisha nyumba yako ina miundombinu ya kukabili moto pamoja na vifaa vya kuzimia moto.Weka vifaa vya kuhisi moto au moshi.

"Hakikisha watu wanaweza kujiokoa kwa kupitia madirishani au kwenye milango ikiwa moto utatokea. Yaani jenga madirisha na milango inayoruhusu watu kujiokoa.Weka vifaa vya kuzimia moto kama vile mpira wa maji wa kuzimia moto pamoja na mitungi ya hewa," anasema.

Anashauri usitumie vitu vinavyoshika moto haraka ikiwamo mafuta ya gari, rangi, gesi, pamba.

"Hakikisha unachunguza kila bidhaa unayotaka kuiweka kwenye nyumba yako ili kubaini kama inashika moto haraka ili ihifadhiwe kwa tahadhari kubwa," anasisitiza.

Jambo lingine analoshauri ni kuchukua tahadhari umeme unapokatika kwa kuzima vifaa vya umeme.


"Tumia vifaa vya kutawala kiwango cha umeme. Hivi huhakikisha umeme unaoingia kwenye vifaa vyako ni wa kiwango kinachotakiwa na huwa na mfumo unaojulikana kama "delay" ambao hauruhusu umeme kuingia kwenye vifaa moja kwa moja mara unaporudi," anashauri.







# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO -
SMS - 0713 447766
PILA SOTOJO TUMELIONA
JUKWAANI
'LITANTOA TOHO!'
'MGAWIO'
SISI
MWAMBIE SHEMELA MUENDE WOTE MKAPIME
LABDA NA 'DIFENDA'
ZAMANI BABU NDIO KIPENZI NA MJUKUU
ZAMA HIZI SIO ZILE TUSIKARIRI MAISHA
MUACHIE MJUKUU AMUITE NCHUMBA!
ATHUBUTUUU!
EMBU ACHENI TOPIKI ZA KICHOCHEZI NA VIJUKUU VTETU!
NYIE! NYIE! NYIE! OHOO!
MIBABU YA SIKU HIZI SIO MIBABU BALI 'MIBABUA'
NIKIENDELEA KUKOSA HELA YA 'VIKAO BAR' NDANI YA MWEZI TU! PEPO NITAKUWA NISHAITEKA
UFUNUO'
TUTAKOROFISHANA KUITANA JINA HILO WE HAYA TU NIMEBADILI JINA
MILUNGI MISHISHA MIB#NG#!
KUSHOBOKEA MIPOMBE MIPYA KABLA KUZIJUA SWAGA ZAKE!
BILA WEWE ILE KESI NINGEFUNGWA
PALE MBELE ULINIONA MIMI BADALA YA HAKIMU! KWELI UCHAWI UPO
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...SIO NGUO TU, HATA SAMAKI ANAVULIWA...

HABARI KIMATAIFA

# Jeshi Burundi laingia Bukavu, wazuia M23 kusonga mbele



Wanajeshi wa Burundi wanadaiwa kuingia Bukavu nchini DRC. **PICHA: AFP**

**GOMA,** DRC

JESHI la Burundi limeingia nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kufanikiwa kuwazuia waasi wa M23 kusonga mbele kuufikia mji wa Bukavu ulioko Kivu Kusini.

Waasi hao wanaoungwa mkono na Rwanda, baada ya kufanikiwa kuuteka mji muhimu wa Goma, wamesonga mbele kuelekea kusini kwa lengo la kuuteka mji huo ambao unapakana na Burundi.

Hata hivyo, jeshi la DRC wakishirikiana na wanajeshi wa Burundi, limedhibiti njia kuu ya kuelekea Bukavu na kuwazuia waasi hao kusonga mbele.

Mapema wiki hii, waasi wa M23 wanaoongozwa na Watutsi waliiteka Goma, mji mkubwa zaidi mashariki mwa DRC ambao ni maarufu kwa migodi ya dhahabu, coltan na madini ya shaba.

Gavana wa jimbo la Kivu Kusini, Jean-Jacques Purusi, alisema vikosi vya jeshi la Congo na Burundi vilifanikiwa kuwadhibiti waasi hao.

Taarifa hiyo ilithibitishwa na vyanzo vingine viwili ambavyo viliiambia shirika la habari la Reuters.

Mmoja wa watu waliokuwa na taarifa za moja kwa moja kuhusu mapigano, alisema kikosi cha wanajeshi takribani 1,500 wakiwemo wanajeshi wa Congo, Burundi, na wapiganaji wanamgambo wa ndani walikuwa wakilinda mji wa Nyabibwe, ulioko kilometa 50 kaskazini mwa Bukavu.

Chanzo hicho kilikataa kutambulika kwa sababu za kiusalama.

### WAKAZI BUKAVU WAJIANDAA

Baadhi ya wakazi wa Bukavu walisema watu walikuwa wanajiandaa kwa kuhifadhi chakula, tochi na betri na wengine kukimbilia mpaka wa Burundi.

Raia waliojitokeza kulinda mji huo walikuwa wakifanya mazoezi kuzunguka uwanja wa michezo na kujipanga kwa ajili ya salamu za kijeshi.

"Tumeumia kwa muda mrefu, tumeumia kwa muda mrefu kwa sababu ya wavamizi ambao ni majirani zetu," alisema mwalimu wa hesabu Habamungu Mushagalusa, mmoja wa kundi la watu takribani 200 walioajiriwa.

"Tuko hapa kulinda ardhi yetu hadi kifo." Alisema mkazi mmoja.

Juzi, Umoja wa Mataifa ulisema kuwa kulikuwa na taarifa za vikosi vya Rwanda kuvuka mpaka na kuelekea Bukavu. Hata hivyo, Rwanda haikujibu ripoti hiyo.

### HOFU YA MZOZO KUENEA

Kuongezeka kwa mzozo huo mashariki mwa DRC kumeibua upinzani kutoka mataifa mbalimbali dhidi ya Rwanda na kutishia uhasama wa kidiplomasia.

"Hatari ya mgogoro kutanuka katika kanda ni halisi," alisema mwanadiplomasia mmoja.

"Majeshi ya Rwanda, DRC na Burundi tayari yanapigana katika ardhi ya mashariki mwa Congo." aliongeza

Ufaransa iliwasilisha rasimu ya azimio katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa juzi ili kuishinikiza Rwanda kuondoa vikosi vyake.

### SADC YAUNGANA NA CONGO

Wakati wa mkutano wa kilele juzi, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) yenye wanachama 16 ilionesha wasiwasi na kuomba kufanya mkutano wa pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu suala hilo.

Pia ilijadili hasara kubwa iliyopata vikosi vyake vya pamoja vilivyokuwepo DRC ambavyo vilipewa jukumu la kuzuia waasi.

Jumuiya hiyo iliomba mawaziri wa ulinzi wa nchi zinazochangia wanajeshi waende DRC kuhakikisha usalama wa vikosi na kurejeshwa kwa majeruhi.

Umoja wa Mataifa ulisema mgogoro huo umeongeza ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwemo mashambulizi dhidi ya watu waliokimbilia kwenye kambi za wakimbizi, mauaji ya kikatili, ubakaji wa kikatili na vitendo vingine vya unyanyasaji wa kingono.

Mkuu wa vikosi vya ulinzi vya Umoja wa Mataifa, Jean-Pierre Lacroix, alisema amani, huduma ya maji na umeme vimerudi katika mji wa Goma ingawa mji bado hali ni tete na yenye kubadilika kila wakati.

Uwanja wa ndege haufanyi kazi kwa sababu ya uharibifu, na walinda amani wa Umoja wa Mataifa walikuwa wakihifadhi raia wengi katika vituo vyao.

Burundi, Uganda zavutwa

Vikosi vya Burundi vinaendelea kuviimarisha vikosi vya DRC, hasa katika mkoa wa Kivu Kusini, kwa ombi la serikali.

Rwanda inadai imekadiria idadi wanajeshi hao kuwa 10,000.

Hata hivyo, Umoja wa Mataifa unakadiria kuwa maelfu kadhaa ya wanajeshi wa Burundi wako Bukavu, ikikadiriwa kati ya 8,000 hadi 10,000.

Umoja wa Mataifa ulisema mapigano kati ya majeshi ya Rwanda na Burundi nchini Congo yanatishia hatari ya vita vya kikanda kama vile vilivyoua mamilioni watu kati ya 1996 na 2003, wengi wao walikufa kutokana na njaa na magonjwa.

Jeshi la Burundi limekataa kutoa tamko kuhusu taarifa ya kuingia DRC.

Uganda ambayo ina wanajeshi mashariki mwa Congo kwa ajili ya kushughulikia waasi,ilisema itatumia mkakati wa kujilinda kutokana na mapigano kati ya jeshi la serikali ya Congo na waasi wa M23.

Mataifa makuu Duniani ikiwamo Marekani, Uingereza na Ufaransa yametoa wito wa kumaliza mapigano nchini DRC na yamejaribu kumshinikiza Rais wa Rwanda Paul Kagame kusitisha msaada wake kwa M23.

Baada ya mkutano na Rais wa DRC, Felix Tshisekedi mjini Kinshasa, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa Jean-Noel Barrot, alikutana na Kagame siku ya pili kutoa ujumbe wa kusitisha vita.

Ofisi ya Rais wa Rwanda ilisema viongozi hao walijadili njia za kuleta amani katika kanda bila kutoa maelezo zaidi.

Wachambuzi wanasema kuwa kukataa kwa mataifa makubwa kuchukua hatua dhidi ya Rwanda, imekuwa changamoto ya kimataifa.

HABARI / MAKALA

# Ujenzi barabara kiwango cha lami kuipaisha Moro

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKARI kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) imetenga Sh. bilioni 320.558 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 189.6 katika Mkoa wa Morogoro ili kukuza uchumi kupitia sekta ya kilimo.

Meneja wa Wakala TANROADS Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Alinanuswe Kyamba, alisema hayo juzi kwenye kikao cha 42 cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Morogoro kilichofanyika mjini hapa.

Mhandisi Kyamba alizitaja barabara hizo na urefu wake katika mabano ni Ifakara- Mbingu (km 62.5), Mbingu- Chita (km 37.5), Bigwa - Mvuha ( km 78) na Ubena Zomozi - Ngerengere (Kizuka Amy Camp) kilometa 11.6.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni 37.841 kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia ili kujenga madaraja maeneo ya Chakwale, Nguyami katika wilaya ya Gairo.

Alitaja madaraja mengine kuwa ni Mjonga, Bwage na Doma yaliyoko katika wilaya ya Mvomero, Ngerengere na Kihonda katika wilaya ya Morogoro.

Mbali na fedha hizo, Mhandisi Kyamba alisema Sh. bilioni 16.153 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa madaraja ya Namhanga na Fuluwa, hivyo kufanya jumla ya fedha kuwa Sh. bilioni 53.994.

Mhandisi Kyamba alisema katika kurejesha mawasiliano katika barabara na madaraja yalioathiriwa na mvua ya EL-nino na kimbunga cha Hidaya, serikali ilitoa kiasi cha Sh. bilioni 4.716.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisema mkoa huo unaweza kupiga hatua zaidi kiuchumi iwapo miundombinu ya barabara itakuwa na ubora wa kupitia msimu wote wa mwaka.

Malima aliitaka TANROADS na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuimarisha miundombinu ya barabara katika maeneo ambayo ni korofi.

Aidha, Mkuu wa Mkoa aliitaka TARURA kushirikiana na mabaraza ya madiwani katika utekelezaji wa bajeti ili kuwa na uelewa wa pamoja.

# Othman ataka misikiti kukuza tabia njema

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wsa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema misikiti inayojengwa katika maeneo mbalimbali nchini inapaswa kuwa mahali sahihi pa ibada, kulea imani na kukuza tabia njema kwa waumini wa Kiislamu.

Othman aliyasema hayo juzi Kijuki Pandani, Kaskazini Pemba, alipowasalimia waumini wa Dini ya Kiislam baada ya kufungua msikiti mpya wa Ijumaa wa Kijiji hicho uliopewa jina la Masjid Nuur Muhammad, alipojumuika nao katika ibada ya swala ya Ijumaa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Habari Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman alisema vyema waumini wakafahamu kwamba wanapaswa kutambua kuwa misikiti si tu kwamba ni mahala pa kufanyia ibada pekee, bali pia inapaswa itumike kuwa sehemu muhimu ya malezi ya nafsi na kitalu cha kukuzia tabia njema ambazo zinapaswa kusomeshwa ndani ya msikitini kwa kufundishwa vijana.

Alisema katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar, kumekuwepo jamii ya vijana kuharibika kitabia na watu kujali kupata tu hata ikiwa ni haramu, jambo linaloathiri mustakabali na jamii kwa kushindwa kujenga imani ya kweli kwa watoto na vijana.

**Makamu wa Kwanza wa Rais alisema mambo wanayofanya watoto na vijana kinyume cha maadili ya jamii na uisilamu ni makubwa kutokana na kuharibikiwa kimalezi. Alisema jamii inapaswa kutimiza wajibu wake wa kuwalea vyema watoto ili kujenga kizazi chema na kuimarisha Uislamu.**

Makamu wa Kwanza wa Rais alisema mambo wanayofanya watoto na vijana kinyume cha maadili ya jamii na uisilamu ni makubwa kutokana na kuharibikiwa kimalezi. Alisema jamii inapaswa kutimiza wajibu wake wa kuwalea vyema watoto ili kujenga kizazi chema na kuimarisha Uislamu.

Aidha, aliwahimiza waumini wa dini ya Kiislamu kutoa swadaka mbalimbali kwa walichoruzukiwa ili kutegemea malipo mema kwa Mola wao aliyewaruzuku mali za aina mbalimbali na kwamba ni vyema pia kushindana katika kutenda mambo mema ili kuipeleka mbali dini yao.

Akitoa salamu za Ofisi ya Mufti, Shekhe Said Ahmed, aliwasihi waumini wa dini ya Kiislamu nchini kutambua kwamba kuwapo kwa neema kujengwa kwa misikiti mipya mizuri, kusilete mifarakano miongoni mwa waumini na badala yake izidishe umoja miongoni mwa waumini na yakitokea hayo, furaha ya misikiti mipya inageuka kuwa huzuni.

Shekhe Said aliwataka Waislamu kutambua kwamba Waislamu wote ni ndugu na ndio msingi wa ibada na dini yao kwa mujibu wa mwongozo wa Mtume Muhammad SAW na kwamba wanapaswa kusaidiana kwa hali na mali ili kufanyiana wepesi kwenye shida na kukingiana mabaya.

Akisoma risala mbele ya mgeni rasmi, Ustadhi Hafidh Said Omar aliwashukuru wafadhili mbalimbali kwa kufanikisha ujenzi wa msikiti huo kwa kipindi cha muda usiozidi mwaka mmoja na kuomba wasaidiwe kifusi cha kuondoa tope katika kipande cha njia ya kuingia kwenye msikiti huo.

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Wazazi wako wamenikataa Selina, piga moyo konde, utapata mwingine



**Na Adam Fungamwango**

MAPENZI ni maridhiano ya watu wawili, kila mmoja akimpenda mwenzake. Watakapopendana bila ushawishi wa mtu yeyote ndio hao watu wanaitwa wapenzi ndiyo maana waswahili wanasema penzi ni ridhaa.

Haiwezekani upangiwe na mtu nani wa kumpenda na nani wa kumwacha kwa sababu mtu anapopenda huwa hana sababu maalum ya kufanya hivyo, badala yake hutokea tu.

Penzi huota kama uyoga tu, bila kujali mazingira yoyote yale.Kinachofanyika mara nyingi ni ushauri tu. Kama kuna tatizo, watu humshauri anayependa kuwa mpenzi wake ni mtu wa aina gani na anatakiwa awe makini na vitu fulani, kama tabia ni mbaya sana atashauriwa amwache. Mpendaji akikataa huwa hakuna chochote kinachoweza kumzuia, badala yake ataachwa ili aende akaone kile ambacho watu walimshauri.

**Siku hizi wanawakataza watoto wao kuoa au kuolewa kwa sababu zisizo na maana kabisa, ikiwemo muonekano na umasikini. Wazazi wanamkataza kabisa binti yao kuolewa na mwanamume ambaye ni maskini, badala yake atafute wa kufanana naye.**

Kwa bahati mbaya sana tangu miaka ya nyuma hadi leo, kuna baadhi ya wazazi huchukua jukumu la kuwakataza watoto wao kuoa au kuolewa na wapenzi wao.

Yaani wao wanampangia mwoaji au mwolewaji, utafikiri ndio wanakwenda kukaa naye.

Afadhali zamani baadhi ya wazazi walikuwa wakiwakataza kwa sababu muhimu kama vile kwenda kwenye familia ya wavivu, wenye magonjwa ya kurithi, yasiyoambukiza na tabia zingine ambazo ni mbaya kwenye jamii.

Siku hizi wanawakataza watoto wao kuoa au kuolewa kwa sababu zisizo na maana kabisa, ikiwemo muonekano na umasikini. Wazazi wanamkataza kabisa binti yao kuolewa na mwanamume ambaye ni maskini, badala yake atafute wa kufanana naye.

Hiyo inatokea sana kwenye familia za watu wanaojiweza kidogo. Wanashindwa kufahamu kuwa binti amempenda mwenyewe na ameridhika kwa kila kitu.

Hata wazazi wa wanaume nao, wako ambao ni wabaguzi. Kijana wao kwenda kuoa familia ya kimaskini wao tabu tupu. Hawataki.

Wengine hawamtaki tu msichana kwa sababu ya mwonekano. Wanaona labda ni mshamba, hana shepu nzuri, haendani na kijana wao, wakati yeye mwenyewe ndiye aliyempenda na anakwenda kuishi naye.

Wako pia wazazi wanaowakataza watoto wao kuoa au kuolewa kwa sababu ya umri. Binti anaweza kumpata mwanamme ambaye umri wake ni mkubwa, inawezekana ni nusu nzima ya umri wake, lakini wazazi wakakataa, licha ya kwamba wenyewe wamependana na kuelewana.

Kijana anaweza kupendana na mwanamke mwenye umri mkubwa kidogo kuliko yeye, lakini kelele zikawa nyingi, kwa nini anamchukua mama mtu mzima, utafikiri wao ndiyo wanaenda kuishi nae.

Kifupi tu ni kwamba jamii, kuanzia wazazi, ndugu, jamaa na marafiki wawe na utamaduni na kuheshimu hisia za wenzao hasa linapokuja suala la mapenzi, Ushauri upo, lakini siyo kuwapiga marufuku.

Mwishoni mwa miaka ya 1970, bendi ya Orchestra Mlimani Park, ilirekodi kibao kiitwacho 'Selina', kilichotungwa na mwanamuziki Joseph Mulenga.

Ilikuwa mwaka 1978 walipoingia studio ikiwa ni albamu ya kwanza ya bendi hiyo tangu ianzishwe.

Kibao hicho kinazungumzia juu ya kijana aliyetaka kumuoa msichana, lakini wazazi wa binti huyo walipinga jambo hilo kwa sababu ambazo zinaonekana zinafanana na hizi tunazozisema.

Baada ya hapo, binti akatishia kutaka kujiua. Kijana aliyetaka kumuoa akamfuata na akawa anambembeleza asifanye hivyo kwa kuwa anaweza kupata mwingine zaidi yake, kwani hayo ni matakwa ya wazazi wake.

"Najua najua una mawazo, lakini tutafanyaje ikiwa wazazi wako wameamua hivyo, najua najua una mawazo, lakini tutafanyaje ikiwa wazazi wako wameamua hivyo.

Nia yangu na madhumuni yangu, nia yangu na madhumuni yangu, ilikuwa tufunge ndoa na tuishi sote kama mke na mume Selina.

"Nimejitahidi kadiri ya uwezo wangu, nimejitahidi kadiri ya uwezo wangu, wazazi wako wamoniwekea vikwazo vingi. Ooh, Selina piga konde moyo ooh, Selina aaa, ooh Selina utafanikiwa ooh Selina aaa.

"Na kwa sababu imekuwa hivyo Selina aaa, sioni haja ya kutaka ujiue, ujinyonge, ujichinje, ujisumbue kwa ajili yangu."

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Nyuma ya Pazia-20

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanaume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamuachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.




****************************************

"Msinidanganye. Bahati nzuri mimi mkinidanganya najua." Alisema na kuwaangalia wote kwa zamu.

"Nani aliwatuma muende Mikwambe kuchukua mkoba wa pesa?" "Malik." Akajibu Pius. "Ni nani huyo?" "Yeye hakukamatwa, tulikuwa wanne, sisi tulikamatwa yeye akakimbia."

Moyoni alikubali kuwa lilikuwa jibu la ukweli. Ni kweli kuna mmoja wao walimuacha akakimbia.

Alikuwa na uwezo wa kumpiga na kumzimisha kama wale wengine, lakini hakutaka kufanya hivyo kwani alijua hawa aliowazimisha wangemtaja mwenzao na pia hawangesema kitu tofauti hata kama angewakamata wote.

Ila alichogundua ambacho hakuweza kukijua kabla kuwa aliyemuacha alikuwa muhimu zaidi. Angejua angehakikisha kuwa haondoki. "Aliwatumaje, au aliwaambiaje?" "Alituambia tumfuate tukachukue mkoba. Hakutuambia wa nini, ila alisema tukifanikiwa kuupata na kumkabidhi yeye, kila mmoja analipwa kiasi cha shilingi laki mbili."

Farjala alidakia. "Kwa hiyo nyinyi hamkujua kwenye ule mkoba kuna nini?" "Haikuwa jukumu letu. Yeye ndiye alituongoza na kusema tuende kumsaidia kuuchukua mkoba ule muda ule wa usiku, dili likifanikiwa tunalipwa hiyo pesa."

"Kwani nyinyi mnafanya kazi ya kwenda kuchukua mikoba ilipowekwa?" Wote watatu walinyamaza na kuangaliana.

Kilichobainika ni kwamba vijana wale ni wahalifu ambao hufanya kazi ya kukodiwa kwenda kufanya matukio mabaya, ya kujeruhi na kuua kwa lengo la kulipwa pesa. Ndiyo maana wote walikuwa na uwezo wa kutumia silaha kama bastola na zile za jadi.

**"Tuma vijana wako waende wakamkamate. Nadhani hapa ndiyo tutakuwa tumefunga ukurasa wa mchezo huu wote. Yeye ndiyo mhusika mkuu, anatuchezea shere"**

"Okay, Fred, chukua hawa warudishe mahabusu mpaka tutakapowahitaji tena." Msaidizi wake akawachukua na kuwarudisha.

Saa 11:00 jioni, kabla hajaondoka, alimpigia simu Mkuu wa Kituo kanda ya Kinondoni. Akaongea naye maneno kadhaa na akamalizia.

"Tuma vijana wako waende wakamkamate. Nadhani hapa ndiyo tutakuwa tumefunga ukurasa wa mchezo huu wote. Yeye ndiyo mhusika mkuu, anatuchezea shere tu," alisema na kumshangaza kamanda. "Umejuaje hili?" Akauliza.

"Nadhani ndiyo maana mlinipa hii kazi na nimeikamilisha, kila kitu kitakuwa wazi kesho," akajibu.

****************************************

Saa tatu asubuhi alikuwa ameshatia timu ofisini. Alikuwa ameshakamilisha kila kitu.

Alikuwa na ushahidi wote mkononi ambao kama angeuwasilisha mahakamani hakuna ambaye angepona.

Aliwaita maafande wote ambao walishiriki katika operesheni hiyo wakati inaanza, lakini ilikuwa ikikwama kwa sababu ya watekaji kupata taarifa ambazo hazijulikani walikuwa wanazipata vipi.

Alimwita pia Mkuu wa Kituo. Mtu ambaye hakuwapo ni Kamanda wa Polisi Kanda ya Kinondoni. Yeye atapelekewa taarifa. Waliletwa pia wale jamaa watatu watekaji waliokuwa mahabusu, Pius,

Farjala, na Said. Wote waliwekwa kwenye ukumbi mmoja ulioonekana kama wa mikutano uliopo kwenye ofisi yake pale Mikocheni.

Eddy alikuwa amemwita pia Macky, baba wa mtoto Macaire ambaye alikuwa ametekwa.

Ndani ya ukumbi huo, aliingizwa mwanamke mmoja ambaye alikwenda kuwekwa kwenye kiti kilichoelekezwa.

Wahusika wote ambao walihitajika walikuwapo. Wengine walishangaana.

Eddy aliingia ndani ya ukumbi huo, ambapo mlangoni kulikuwa na askari polisi mmoja mwenye silaha akilinda na mwingine akivaa kiraia.

Aliwasalimia maafande na akaenda kumsalimia Macky. Kiti chake kilikuwa mbele, pamoja cha Mkuu wa Kituo Polisi kanda.

Ni wao wawili tu waliokuwa na viti mbele. Baada ya dakika moja hivi kupita, Eddy alimtazama Macky.

"Macky, mpaka sasa hujajua mtoto wako yuko wapi?" "Hapana ndugu mwandishi." Akajibu. "Yupo kwa mama yake." Akajibu kwa kifupi, kitu ambacho kilimshangaza Macky.

"Amerudishwa lini?" Akauliza. "Hakurudishwa. Ndiko alikokuwa tangu mwanzo." Ni jibu ambalo halikumshangaza Macky tu, bali wengi waliokuwamo mule.

"Ni hivi, ngoja nieleze mchezo mzima ulivyo. Ni kwamba mtoto huyu hakutekwa. Kuna mchezo mmoja umefanyika kwa ajili ya kujipatia pesa. Kuna maigizo yamechezwa hapa." Eddy bado alizidi kuwaweka njia panda wasikilizaji.

"Mnakumbuka kamanda mlinipa kazi hii, kwanza kabisa kujua ni watu gani, au ni nani waliyemteka mtoto. Pili kuwatia mbaroni.

Tatu kujua ni kwa nini siri zilikuwa zinavuja pindi polisi walipokuwa wakiweka mtego wa kuwakamata watekaji wanapokuwa wanataka pesa kwa ajili ya kuachiwa mtoto.

Nne ni kumjua aliye nyuma ya mpango huu wote. Hapa nilipo tayari nimeshajua kila kitu na nina ushahidi.

Kwanza kabisa namleta kwenu mtekaji wa mtoto Macaire ni mama yake mwenyewe, Dora, akishirikiana na bwana wake anayeishi naye, Malick.

Pili, siri zilikuwa zinatoka kwa sababu mama mzazi alikuwa anashirikishwa na polisi kwenye mpango wa kuwatumia pesa watekaji ili wamuachie mtoto, kwa maana hiyo alikuwa anawasiliana na mpenzi wake kuwa wasiende walikoeleza zipelekwe kwa sababu kuna mtego wa polisi.

Mara mbili watekaji wameshindwa kunaswa na polisi kwa sababu taarifa zilikuwa zinapelekwa na Dora, mama mzazi wa mtekwaji.

Ndiyo maana hata pesa zilipoenda kuwekwa, watekaji walikuwa wakimpigia simu baba mzazi wa mtoto kuwa wamegundua kuwa kuna mtego na kumtaka arudi na pesa zake.

Ni zile ambazo polisi walikuwa wanazitoa kama mtego." Kila alipokuwa akiendelea ndiyo kisa hicho kilivutia watu wengi waliokuwa ndani ya ukumbi huo, na kuwaogopesha wengine.


"Nakumbuka mara ya kwanza mtego uliwekwa maeneo ya Bonde la Kinondoni Mkwajuni, lakini Macky akirejea na pesa alizopewa na jeshi la polisi, na wa pili ulikuwa ni kwenye daraja lililopo barabara ya Kawawa, kwenye kibonde kidogo kati ya Magomeni Mikumi na kwenye 'raundi abauti' ya barabara ya Kigogo. Mitego yote ilifeli.

Jeshi la Polisi, kupitia wewe Mkuu wa Kituo Kanda ya Kinondoni, ukaanza kushuku kuwa huenda baadhi ya askari wako wanashirikiana na watekaji kuvujisha siri ili wasikamatwe.

Awali aliyehisiwa alikuwa ni Mwalimu Mkuu wa shule ya Tom Academy, ambayo mtoto Macaire alikuwa akisoma, Dickson Kisanga, kuwa huenda anaweza kuwa alishirikiana na watekaji na akawa anavujisha siri.

Hakushirikishwa mpango wa pili wa kupeleka pesa, lakini hali ikawa ile ile.

**Itaendelea Jumapili**



# DE MASTER AOMBA MASHABIKI KUMSAPOTI

**Na Halfani Chusi**

MSANII wa muziki wa kizazi Kipya, Deo Meta maarufu De Master, amewaomba mashabiki zake wamuunge mkono kupitia wimbo wake mpya aliouachia hivi karibuni.

De master aliliambia gazeti hili jana kwamba mbali na wimbo huo, anaandaa mwingine anaotarajia kuuachia siku chache zijazo.

"Mashabiki zangu nipo kitambo kwenye gemu, ninafuata nyayo za mama yangu ambaye pia alikuwa msanii wa nyimbo za asili, ninaomba mnipokee ngoma yangu inayokwenda kwa jina la kichomi ipo hewani na inapatikana katika mitandao yangu yote ya kijamii," amesema.

"Nina uwezo wa kutunga na kuandika kama mtu atajitokeza kunisapoti tunaweza kukaa tukafanya kazi nina uhakika sitomuangusha" ameongeza De Master

# Wasanii wapewa fursa

WASANII wa Tanzania wamepewa fursa kupatiwa ufadhili wa kuendeleza vipaji vyao vya sanaa.

Ufadhili huo wa fedha wa kiasi cha milioni 17, umetolewa na kituo cha kuendeleza sanaa cha Nafasi Art Space cha jijini Dar es Salaam na unawalenga wasanii wa fani mbalimbali.

Kupitia mradi wao wa 'Feel Free Grant', uko wazi kwa msanii yeyote mwenye maono ya kiubunifu kutekeleza mradi wake hapa nchini.

Kituo hicho kilisema lengo la mradi huo ni kuwafanya wasanii wenye vipaji kuichangamkia fursa hiyo ambayo itaongeza kupata mabadiliko ya namna mpya za kiubunifu.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RASHFORD AKWAMA BARCA

JARIBIO la Barcelona kumsajili fowadi wa Manchester United, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27 limeshindikana kwa sababu hawajauza wachezaji wa kutosha ili kupata fedha. ***(ESPN)***

### AMORIMI ALIA NA USAJILI

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim, amesikitishwa na klabu hiyo kwa kutokuwanunua wachezaji wapya katika dirisha dogo la usajili lililomalizika hapo Januari. ***(Manchester Evening)***

### BROBBEY MKATABA MPYA

WEST Ham imeambiwa itahitaji kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Brian Brobbey, mwenye umri wa miaka 22, kwa mkataba wa kudumu kwa sababu Ajax hawajaonesha nia ya kumtoa kwa mkopo. ***(Fabrizio Romano)***

### MADRID, KIMMICH WATETA

REAL Madrid imeanza mazungumzo ya mapema na kiungo wa kati wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Joshua Kimmich, mwenye umri wa miaka 29, kuhusu uhamisho wake, mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu. ***(Bild)***

### ZINCHENKO BADO YUPO

ARSENAL haikupokea ofa yoyote ya kumuuza mchezaji wake, Oleksandr Zinchenko, mwenye umri wa miaka 28. ***(Sky Sports)***

### TOMORI ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo kwenye mazungumzo yaliyofikia hatua kubwa kwa ajili ya kumsajili beki wa England, Fikayo Tomori, mwenye umri wa miaka 27 kutoka AC Milan. ***(Sky Sports)***

### TEL AIKATAA SPURS

MCHEZAJI, Mathys Tel, amekataa kuhama kutoka Bayern Munich na kujiunga na Tottenham baada ya klabu hizo kuafikiana kuhusu ada ya pauni milioni 50.1 kwa ajili ya mshambuliaji huyo Mfaransa mwenye umri wa miaka 19. ***(ESPN)***

### CITY: GONZALEZ HAONDOKI

KLABU ya Manchester City haiko tayari kutimiza masharti ya pauni milioni 50 kwa Gonzalez kabla ya tarehe ya mwisho ya kuhama. ***(Telegraph)***

### AL NASSR YAKWAA KISIKI

KLABU ya Brighton imekataa ofa iliyoboreshwa ya pauni milioni 75 kutoka kwa Al-Nassr ya Saudi Arababi ili kumsajili winga raia wa Japan, Kaoru Mitoma, mwenye umri wa miaka 27. ***(Sun)***

### DARWIN KUBAKIA LIVER

NYOTA Darwin Nunez alitaka kuzungumza na Al-Nassr kabla ya kumsajili, Jhon Duran, lakini Liverpool wakawaambia mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Uruguay mwenye umri wa miaka 25, hauzwi kwa bei yoyote. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBWEMBWE ZATAWALA NEYMAR AKITUA SANTOS

## Mashabiki wake wapagawa 'mfalme wao' akitambulishwa...

**SANTOS,** Brazil

NEYMAR akiwa analia machozi alikaribishwa katika klabu yake ya utotoni mbele ya maelfu ya mashabiki wa Santos waliohudhuria tamasha lililofanyika kwenye uwanja wa nyumbani wa timu hiyo chini ya maandishi ya kielektroniki yaliyosomeka, "mfalme amerudi."

**Mshambuliaji huyo alitia saini mkataba wa miezi sita, kwa mujibu wa ESPN.**

Takriban mashabiki 20,000 wa Santos waliujaza Uwanja wa Vila Belmiro ulioko nje ya jiji la São Paulo ili kusherehekea kurejea kwa Neymar mwenye umri wa miaka 32, licha ya kuwapo na mvua.

Kufika kwake jioni kwa fataki kulikamilisha sherehe ya saa tatu ambayo pia ilishirikisha wanamuziki kadhaa.

"Nina furaha sana. Tuliishi nyakati nzuri hapa. Bado kuna mengi yanayoweza kuja," alisema Neymar uwanjani hapo.

Mashabiki walipoimba wanataka kumwona akipiga chenga tena, kama alivyokuwa akifanya mara nyingi katika uchezaji wake, alisema, "Sitakosa ujasiri wa kupiga chenga."

Muda mfupi kabla, aliwasalimia wachezaji wenzake wa baadaye na watendaji wa klabu hiyo kwenye uwanja wa mazoezi wa Santos.

Ndege binafsi ya Neymar ilitua katika eneo la mashambani la Jimbo la São Paulo kutoka Saudi Arabia asubuhi, lakini aliomba saa chache za kupumzika kabla ya kusafirishwa hadi Santos kwa helikopta.

Mabango yaliyosomeka "mfalme amerudi" yalikuwa yakiuzwa kwa reais 10 (sawa na dola 1.50).

Video iliyotumwa na Santos kwenye mitandao ya kijamii ilionyesha Neymar hajavaa nambari 11 ambayo ilikuwa yake wakati wa kipindi chake cha kwanza kutoka kati ya mwaka 2009 na 2013.

Na sasa atavaa jezi namba 10 ya Pele katika kipindi chake cha pili katika klabu hiyo.

"Itakuwa heshima kuvaa jezi hii takatifu," alisema Neymar kwenye video hiyo.

Klabu ya Saudi Pro League ya Al Hilal ilitangaza Jumatatu iliyopita imefikia makubaliano na Neymar kusitisha mkataba wake baada ya nyota huyo wa Brazil kufunga bao moja katika mechi saba katika kipindi cha miezi 18.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona aliumia misulu ya paja ya goti lake la kushoto alipokuwa kwenye majukumu ya kimataifa muda mfupi baada ya kusajiliwa na Al Hilal.

Alirejea uwanjani Oktoba, mwaka jana lakini jeraha la misuli ya paja lilimzuia kutoa mchango mkubwa kwa klabu. Neymar aliulizwa katika mkutano na waandishi wa habari kutaka kurejea Santos.

"Kuna baadhi ya maamuzi yanaenda nje ya mantiki ya soka, na mengine yana athari," alisema.

# AMORIM AFURAHISHWA UWEZO WA GARNACHO

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim amemsifu, Alejandro Garnacho, kwa uchezaji wake wa hivi karibuni, akidai winga huyo "amebadilisha kila kitu" ili kujipatia faida.

Ni wiki saba zimepita tangu Garnacho na mhitimu mwenzake wa akademi, Marcus Rashford, kuachwa kwa mshangao katika kikosi cha United waliporejea na kuifunga Manchester City mabao 2-1.

Tangu wakati huo, Rashford amekosa katika vikosi 11 vilivyofuata na ametawala vichwa vya habari huku Garnacho akihusishwa na kuondoka.

Garnacho alivutia tena baada ya kuingia kama mchezaji wa akiba katika ushindi wa mabao 2-0 kwenye Ligi ya Europa dhidi ya Steaua Bucharest Alhamisi iliyopita na Amorim alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina anastahili sifa.

"Alibadilika mara moja kutoka mechi dhidi ya City," alisema bosi huyo wa United.

"Jinsi anavyoelewa mambo na kuelewa nataka kumsaidia, nataka tu kushinda michezo. Alibadilika kwa kila kitu, mtazamo wakati nazungumza naye, jinsi anavyopona.

"Anaelewa wakati mwingine mimi ni kocha tofauti, ninadai kwa njia yangu, wakati mwingine ni ngumu matokeo ya kwanza. Ni aina tofauti ya kocha na anaelewa sio kwa njia mbaya, ni kwa ajili yake kila wakati. lakini mimi ni mtu tofauti.

"Nadhani sifa zote ni kutoka kwa Garnacho na anaimarika, na tunataka kuendelea kuimarika na Garnacho."



# Guardiola amtaka Rodri asijilazimishe

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amemshauri staa wa timu hiyo Rodrigo kutoharakisha kuwahi uwanjani na badala yake atumie muda huu kujiimarisha zaidi.

Guardiola amesema licha ya nyota huyo kuwa na mchango mkubwa katika kikosi chake anatamani arejee akiwa kamili ili aepuke kukaa tena kwenye majeraha kwa muda mrefu.

Rodri, raia wa Hispania na mshindi wa tuzo ya Balon D'or alipata majeraha katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Arsenal mchezo ambao ulimalizika kwa sare ya 2-2 Septemba, mwaka jana.

Mchezaji huyo alisafiri na kikosi kuelekea Paris kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya PSG mapema mwezi huu, na tangu mUda huo amekuwa akionekana kwenye mechi na mazoezi ya Manchester City jambo lililozua tetesi huenda akawa sehemu ya kikosi hicho kitakachocheza hatua ya 16 bora ya UEFA.

"Yuko vizuri japo siwezi kuthibitisha hilo, jeraha ni jeraha siku zote naamini kwenye majeraha ni muhimu sana kuheshimu muda, ni vyema kuwa nae tena uwanjani, mazoezini na sehemu nyingine lakini natamani atulie, kitu muhimu sana kwake ni kupona" amesema Pep.

Baada ya upasuaji wa Rodri, jijini Madrid taarifa zilieleza anahitaji muda mrefu zaidi kupona ikikadiriwa huenda asicheze kabisa msimu huu lakini kasi ya kupona kwake iliibua taarifa nyingine za huenda akarejea kabla ya muda uliotegemewa.





# *Al Nassr yakwama kumsajili Mitoma*

**LONDON,** England

TIMU ya Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Al Nassr wamesitisha rasmi majaribio ya kumsajili winga wa Brighton, Kaoru Mitoma, baada ya klabu yake hiyo kukataa dau la euro milioni 65 huku wakitarajia dau kubwa zaidi.

BBC sport imeripoti katika mazungumzo zaidi baina ya klabu hizo, Brighton waliweka wazi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 hauzwi na hawako tayari kubadili msimamo wao juu ya kumbakiza hata iweje jambo lililopelekea Al Nassr kukubali yaishe.

Mitoma amecheza michezo 92 tangu awasili Amex stadium kutoka Kawasaki Frontale (Ligi Kuu Japan ), mwaka 2021 na tayari akiwa amecheka na nyavu mara 18.

Mjapani huyo anasalia mchezaji pekee wa Brighton kucheza michezo yote 23 ya Ligi Kuu England huku kikosi hicho cha Fabian Hurzeler kikikamatilia nafasi ya tisa kwenye ligi hiyo.

Oktoba mwaka juzi, Mitoma aliongeza mkataba wa kuendelea na klabu hiyo hadi mwaka, 2027.

# MAJALIWA AFUNGUKA UBORA SOKA JUU, AHIMIZA MAZOEZI

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akihimiza wananchi kushiriki kufanya mazoezi mbalimbali kwa lengo la kuimarisha afya zao, amesema kwa sasa Tanzania imepanda kwa ubora katika mchezo wa soka.

Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), imefuzu kwa mara nyingine kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ambazo zitafanyika baadaye mwaka huu nchini, Morocco, ikiwa imepangwa Kundi C pamoja na Tunisia, Nigeria na Uganda.

**Waziri Mkuu, Majaliwa alisema hayo jana jijini, Dodoma katika Bunge Bonanza, ambalo lilishirikisha mashabiki wa Simba, Yanga, wabunge na viongozi kutoka taasisi mbalimbali.**

Alimpongeza Spika wa Bunge, Dk. Tulia kwa kuanzisha wazo hilo la kuandaa bonanza kwa sababu linasaidia kuongeza hamasa ya kushiriki katika michezo kwa viongozi na wadau.

Alisema bonanza ni chanzo kimojawapo cha kuibua vipaji mbalimbali vya wachezaji na mkakati huo umeenda mbali kwa nchi kupata mafanikio makubwa.

"Huu ni utamaduni uliobuniwa na Spika wetu, Dk. Tulia pamoja na katibu wetu, inapanua wigo wa kuhamasisha urafiki, huu ni mkakati ambao leo hii nchi yetu inaendelea, wote ni mashabiki, kwa upande wa soka tumeenda mbali sana," alisema Majaliwa.

Aliongeza michezo sio tu inaleta furaha, pia inaongeza urafiki na watu wanapata nafasi ya kuonyesha vipaji vyao.

"Leo (jana), tumeanza kwa kutembea kilomita tatu, lakini pia sasa hivi tumeona riadha imechezwa, kuna mpira wa kikapu, wavu, netiboli imechezwa, pia tumeona power Chila akivutana na watu 50," Majaliwa alisema.

Alitaja baadhi ya michezo mingine ambayo ilitarajiwa kuchezwa katika bonanza hilo ni pamoja na mbio za magunia, kukimbia na mayai pamoja na kuvuta kamba.

Kwa upande wa soka, mashabiki wa Simba walipata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya watani zao, Yanga katika mechi iliyochezwa mapema jana asubuhi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati), akiwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), katika mbio za kilomita tatu kwenye Tamasha la Bunge Bonanza lililofanyika jijini, Dodoma jana. **PICHA: MTANDAO**

## Zimamoto yatamba ikiwaalika Mlandege

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Zimamoto, Mohamed Hilali, amesema amejiandaa kuendeleza historia yake ya kuifunga Mlandege FC kama alivyofanya katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar.

Zimamoto itaikaribisha Mlandege leo katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa kwenye Uwanja wa Cairo ulioko eneo la Kiwengwa Kisiwani. Hilali alisema anafahamu wapinzani wake watajiandaa kupambana na kutorudia makosa ili kuepuka kichapo.

"Mpango wetu mkubwa ni kuendelea kuwanyanyasa matajiri hawa Mlandege FC, tunaamini ndani ya dakika 90 tutacheza kwa utulivu na hatutakuwa tayari kuingia katika mtego wao, nitawakumbusha wachezaji wangu kuongeza umakini hasa tunapokuwa tunashambuliwa na pale tukiwa tunamiliki mipira," alisema kocha huyo.

Aliongeza amekiandaa kikosi chake vizuri kwa kuyafanyia kazi mapungufu yote aliyoyaona katika mzunguko wa kwanza ili kuwa imara tayari na mapambano wakati wa lala salama.

## Polisi, Yellow Jacket hapatoshi Februari 8

**Na Onesmo Kapinga**

TIMU ya kikapu ya Polisi inatakutana na Yellow Jacket katika mchezo wa robo fainali ya Ligi Daraja la Kwanza Mkoa wa Dar es Salaam itakayochezwa Februari 8, mwaka huu kwenye Uwanja a Bandari hapa, jijini.

Polisi itaingia uwanjani ikihitaji ushindi baada ya kuongoza katika mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo kutokana na kufikisha pointi 34, ikiwa imecheza michezo 17.

Wapinzani wao Yellow Jacket wao wanahitaji kusahihisha makosa kwa kupata ushindi ili wasonge mbele hatua inayofuata baada ya kukaa katika nafasi ya nane kwenye msimamo ikiwa na pointi 27 kibindoni.

Katika mfululizo wa ligi hiyo, Stein Warriors iliyoshika nafasi ya pili ikiwa na pointi 32, yenyewe itamenyana na Kigamboni Heroes yenye pointi 27.

Mechi nyingine ya hatua ya robo fainali itawakutanisha Kurasini Heat dhidi ya Mbezi Beach huku Chang'ombe Warriors yenye pointi 29 ikijipanga kukutana na Mlimani B.C. Bingwa wa ligi hiyo ataiwakilisha Dar es Salaam katika mashindano ya taifa yatakayofanyika baadaye mwaka huu.

## *Sare yaikera Uhamiaji Ligi Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kutoka suluhu na Malindi, Kocha Mkuu wa Uhamiaji, Abdulsalehe Abdallah, amesema imewapunguza kasi katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza ya ligi hiyo, Uhamiaji iliichapa Malindi mabao 3-0.

Abdulsalehe alisema alijua mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sabau ya uhitaji wa kupata pointi ulivyokuwa kwa pande zote mbili.

Kocha huyo alisema kila timu ilifanya maandalizi mazuri na makubwa kutokana na mapumziko marefu waliyoyapata na walitarajia kukutana na ushindani katika mchezo huo.

"Tulicheza vizuri, ingawa mchezo wenyewe ulikuwa na 'tension' kubwa kuanzia kwa wachezaji, mashabiki na hata viongozi, huu ni mchezo wa kwanza kwa mzunguko huu hivyo kila mmoja mpango wake ni kupata pointi tatu," alisema Abdusalehe.

Kocha Msaidizi wa Malindi, Suleiman Mohamed, alisema pointi moja waliyopata ni kubwa kwao kutokana na matokeo waliyopata walipokutana katika mzunguko wa kwanza msimu huu.


"Wachezaji waliingia uwanjani kwa lengo la kuondoka na alama tatu, lakini mipango yetu ilifanana, na hata kuzidiana mbinu mpaka kupata matokeo haya ya sare," alisema Suleiman.

Wakati huo huo, mechi nyingine ya ligi hiyo iliyotarajiwa kuchezwa mapema jana mchana kati ya KMKM SC dhidi ya Inter Zanzibar haikufanyika kutokana na Inter Zanzibar FC kuchelewa kufika uwanjani.

Michezo

Jumapili Februari 2, 2025

Nipashe



Guardiola amtaka Rodri asijilazimishe UKURASA 22




Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize (kulia), akijipanga kupiga shuti huku akikabwa na beki wa kati wa Kagera Sugar, Samuel Onditi, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana. Yanga ilipata ushindi wa mabao 4-0. **PICHA: YANGA SC**

# Yanga yapaa kileleni

## ●●● 'Yaibugiza' Kagera Sugar 4-0, Mzize...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi, Yanga wamekaa kileleni baada ya kuwaangamiza Kagera Sugar mabao 4-0 katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana.

**Ulikuwa ni ushindi wa sita mfululizo kwa Yanga tangu ilipopoteza kwa kufungwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United, Novemba 7, mwaka jana, pia ikiwa chini ya Kocha Mkuu, Mjerumani, Sead Ramovic.**

Ushindi huo unaifanya Yanga kufikia pointi 42 baada ya kucheza michezo 16, ikishinda mechi 14, ikipoteza miwili, huku ikiendelea kuwa timu pekee ambayo haijapata sare yoyote mpaka sasa msimu huu.

Hata hivyo, kuendelea kujidai kileleni kwa Yanga kutatokana na matokeo ya mchezo wa leo, kati ya Simba itakayoshuka ugenini kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora kuvaana na wenyeji, Tabora United.

Iwapo Simba itashinda, Yanga itashuka tena kwenye nafasi yake ya pili, lakini itaendelea kutamba kileleni kama Wekundu wa Msimbazi, wenye pointi 40, watapoteza au kutoka sare.

Katika mchezo huo, shambulizi la kwanza lilianza dakika ya pili ya mchezo, Yanga ikiingia ndani ya eneo la wapinzani wao kwa mpira uliporwa na Mudathir Yahaya kutoka kwa mabeki wa Kagera Sugar, akaupeleka kwa Stephane Aziz Ki, ambaye shuti lake lilionekana linajaa ndani ya nyavu na mashabiki kunyanyuka, lakini lilitoka juu kidogo ya lango.

Shambulizi lingine la hatari lilifanywa na Yanga dakika ya 15, wakati Aziz Ki, alipowatoka mabeki wa Kagera Sugar, akammegea, Clement Mzize ambaye shuti lake lilitoka pembeni kidogo ya lango.

Mabeki wa Kagera Sugar wakijitahidi sana kuzima mashambulizi ya Yanga upande wa kushoto kutoka kwa Shadrack Boka.

Akishirikiana na beki wake wa kati, Abdallah Mfuko, walifanya kazi ya ziada na kama si uzembe wa baadhi ya wenzao, mechi hiyo ingeenda suluhu mapumziko. Hata hivyo kazi hiyo ilifanikiwa kipindi cha kwanza tu.

Mzize aliwanyanyua mashabiki wa Yanga dakika ya 31, waliokuwa wamekaa muda wote wakiwa hawaelewi, alipopachika bao la kwanza lililotokana na makosa ya mabeki wa Kagera Sugar ambao walianza mpira kizembe ambao ulinaswa, ukapelekwa kwa Aziz Ki, ambaye hakuwa mchoyo, anamwekea mfungaji huyo aliyekuwa katika nafasi nzuri ya kupachika bao.

Lilikuwa ni bao la saba kwa Mzize msimu huu, lakini wakishuhudia Aziz Ki, akikosa penalti dakika ya 35, kufuatia kipa wa Kagera Sugar, Ramadhani Chalamanda, kuipangua na ulipotua katika mguu wa kulia wa Israel Mwenda, alipiga nje.

Penalti hiyo ilitolewa na mwamuzi, Nassor Mwinchui, baada ya Hijja Shamte, kumwangusha Mudathir Yahya, ndani ya eneo la hatari.

Kipindi cha pili ndipo dhahama ilipowaangukia Kagera Sugar, Mudathir alipachika mpira wavuni dakika ya 59, kufuatia kuunganisha vyema krosi ya Prince Dube huku Pacome akifunga bao la tatu dakika ya 77, baada ya mwamuzi, Nassor Mwinchui, kutoa penalti nyingine, pale, Maxi Nzengeli alipoangushwa ndani ya eneo la hatari.

Kennedy Musonda alifunga bao la nne dakika tano kabla ya mchezo kumalizika akiunganisha krosi kutoka wingi ya kulia, iliyotokana na kona fupi ambayo iligongwa na wachezaji kadhaa kabla ya kumiminwa langoni, mfungaji akitumia tena makosa ya walinzi wa Kagera Sugar na Chalamanda kutegeana kuondoa hatari hiyo.

Kagera Sugar yenye pointi 11 inaendelea kubakia nafasi ya 15 ya msimamo wa Ligi Kuu.

# Simba, Tabora Utd mwisho wa tambo

**Somoe Ng'itu na Adam Fungamwango**

KUCHEZA kimkakati ili kupata ushindi ndio jambo muhimu kwa Simba kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji Tabora United itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, alisema jana wamejipanga kuikabili Tabora United 'kimkakati', kwa sababu wanafahamu ni timu nzuri na iliyoimarika zaidi kwa sasa.

Fadlu alisema wamejiandaa kucheza kwenye uwanja ambao ana wasiwasi hautafanya wawe na uhuru wa kumiliki vyema mpira kwa kiasi kikubwa.

Kocha huyo alisema kikosi chake kipo tayari kukabiliana na kila aina ya ushindani katika mchezo huo kwa sababu wako imara kwa ajili ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika pamoja na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ujumla na si kwa ajili ya Tabora United pekee.

"Kwanza kabisa tulikuwa tunajiandaa kwa ajili ya mechi za Kombe la Shirikisho na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu na wala siyo kwa ajili ya Tabora United, lakini pamoja na hayo tunaiheshimu sana, ina wachezaji wazuri, ila tutakwenda kucheza kama tunacheza na timu nyingine, lakini uwanja nao unaweza kutuamulia mfumo ambao tutatakiwa kucheza, najua hauwezi kutupa uhuru sana kama inavyokuwa Benjamin Mkapa au KMC Complex," alisema Fadlu.

Aliongeza kutokana na hilo mechi hiyo itachezwa kimkakati zaidi, huku akiwa ameshajua maeneo hatari ya wapinzani wao yanapotokea.

Kocha Mkuu wa Tabora United, Anicet Kiazayidi, alisema tayari maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na wachezaji wake wapo fiti, anachosubiri ni dakika 90.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042